# Kukuza Ujifunzaji Mahiri Darasani

**Moduli**

**6**



## Mwongozo wa Mkufunzi

SMZ
SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME

NAD – The Norwegian Association of Disabled

EENET Enabling Education Network

# Kukuza Ujifunzaji Mahiri Darasani

## Moduli ya Sita

### Mwongozo wa Mkufunzi

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar
S.L.P 840,
Mazizini,
Zanzibar
info@zie.go.tz
www.zie.go.tz
Simu: +255-24-2230193

Toleo la Kwanza, 2023

Umetayarishwa na Enabling Education Network Machi, 2018

TEZ, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2023

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kwa ajili ya kuuza bila ya ruhusa ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ). Matumizi yoyote ya toleo hili kwa kunakili, kutafsiri na kukitoa kwa njia ya kielektroniki bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu ni kosa la kisheria na utashitakiwa.

Kazi hii imepewa leseni chini ya Creative Common Attribution – Shirika lisilo la kibiashara- 4.0 Leseni ya Kimataifa. Ili kuona kivuli cha leseni, tembelea
http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Dibaji

Moduli hii ya Elimu Mjumuisho inalenga kuweka mazingira yaliyosawa ili kuhakikisha kila mtu anashiriki vyema katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Utayarishwaji wa moduli hii ya elimu mjumuisho utasaidia kufikia malengo yaliyowekwa katika mkutano wa Jomtien nchini Thailand (1990) ambako UNICEF ilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa nchi zichukue hatua za kuondokana na tafauti za elimu zinazojitokeza miongoni mwa makundi ya vijana wenye mazingira magumu. Vile vile, utayarishwaji huu wa Moduli hii ya elimu mjumuisho ni matokeo ya:

- Warsha ya mafunzo ya wakufunzi iliyotayarishwa na Diakonia, Palestina, Julai 2011.
- Elimu Mjumuisho: Mwongozo wa wakufunzi wa walimu, uliyotayarishwa na Shirikisho la Kimataifa la Ulemavu (HIF), Cambodia, 2011.
- Programu ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa na Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), Macedonia, 2012–13.
- Programu ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa na UNICEF, Libya, 2012–2013.
- Utangulizi wa Elimu Mjumuisho: 'Mwongozo wa Wakufunzi' ulioandaliwa na HIF, Liberia, 2012–13.

Napenda kutambua mchango wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ya Norway (NAD) na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili (NFU) katika kusaidia kuandika moduli za elimu mjumuisho na kuhakikisha kuwa zinamuongoza vyema mwalimu katika kukidhi mahitaji ya Elimu Mjumuisho. Aidha, napenda kutambua mchango wa Jumuiya ya Makuzi ya Awali ya Mtoto-Zanzibar (MECP-Z) kwa kusimamia upitiaji wa moduli hizi. Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha Zanzibar kwa kuzifanyia majaribio moduli zote kwa hatua ya awali.

Ni matarajio yetu kuwa moduli za elimu mjumuisho zitatumika katika kuwaongoza walimu kukabiliana na mazingira jumuishi Zanzibar. Vile vile, wakufunzi wa vyuo vya ualimu na wahadhiri wa nyuo vikuu watatumia miongozo hii kwa ajili ya kuhakikisha walimu wanapata uzoefu katika kukabiliana na mazingira ya elimu mjumuisho Zanzibar.

__________________________

Khamis Abdulla Said
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
**Zanzibar.**

# Shukurani

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) inatoa shukurani za dhati kwa taasisi mbalimbali zilizohusika katika kutayarisha na kupitia Moduli hii ya Elimu Mjumuisho. Taasisi hizi ni pamoja na Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha Zanzibar, Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Vyuo vya Ualimu vya Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Aidha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Jumuiya ya Makuzi ya Awali ya Mtoto Zanzibar (MECP-Z) zimehakikisha kuwa moduli zilizotayarishwa zinamuongoza vyema mwalimu katika kukidhi mahitaji ya mazingira ya Elimu Mjumuisho.

Aidha, Wizara inawashukuru  wote waliotayarisha Moduli na zana zote na kuzifanyia majaribia kwa ushirikiano na wafanyakazi wa Mtandao wa Kuwezesha Elimu (EENET) na washauri kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika, Asia na Ulaya kwa kipindi cha miaka 10 au zaidi.

Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa wafadhili wa elimu Zanzibar kupitia Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ya Norway (NAD) kwa kuendelea kushirikiana na WEMA katika kufanikisha uandaaji wa mwongozo huu.

____________________

Abdallah M. Mussa
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.

# Yaliyomo

Vifupisho ........................................................................................ 8
Utangulizi ........................................................................................ 9

Kipindi cha 6.1: Ahadi yetu katika kuuendea mjumuisho ................................ 11
Kipindi cha 6.2: Kuandaa mazingira ya ujifunzaji mahiri ................................ 17
Kipindi cha 6.3: Kukuza shughuli za kushajihisha ujifunzaji mahiri .................... 26
Kipindi cha 6.4: Kupanga na kuendesha kazi ya kikundi .................................. 32
Kipindi cha 6.5: Tumia utafautishaji katika madarasa yenye wanafunzi wenye uwezo tafauti ........................................................................ 40
Kipindi cha 6.6: Kutumia tathmini ili kusaidia ujifunzaji .................................. 54
Kipindi cha 6.7: Kutumia utafiti tatuzi ili kukuza ujifunzaji mahiri ..................... 62

Kielelezo nambari 6.1 Majibu tendaji na yasiyo tendaji .................................. 65
Kielelezo nambari 6.2: Taarifa tendaji na zisizo tendaji .................................. 66
Kielelezo nambari 6.3: Kadi ‘za dira yetu’ ...................................................... 67
Kielelezo nambari 6.4: Kutambua malengo yetu ............................................ 68
Kielelezo nambari 6.5: Picha za darasani ....................................................... 69
Kielelezo nambari 6.6: Kujibu picha za darasani ............................................. 72
Kielelezo nambari 6.7: Mabadiliko yanayopendekezwa .................................. 73
Kielelezo nambari 6.8: Kuandaa mazingira halisi ya darasa ............................ 74
Kielelezo nambari 6.9: Kuandaa mazingira darasani kisaikolojia na kijamii ....... 76
Kielelezo nambari 6.10: Video ya EENET ‘Siku ya mjumuisho’, Mpango wa 7 juu ya ufundishaji na ujifunzaji ............................................................ 78
Kielelezo nambari 6.11: Dondoo muhimu kutoka kwenye nakala ya video ...... 79
Kielelezo nambari 6.12: Mbinu za kujifunza kwa vitendo ................................ 81
Kielelezo nambari 6.13: Malengo ya ujifunzaji ............................................... 82
Kielelezo nambari 6.14: Mikakati ya ujifunzaji mahiri ..................................... 84
Kielelezo nambari 6.15: Faida na changamoto za kazi ya kikundi .................... 85
Kielelezo nambari 6.16: kupanga muundo wa kila kikundi .............................. 86
Kielelezo nambari 6.17: Orodhahakiki ya kupanga kazi ya kikundi bora ........... 87

Kielelezo nambari 6.18: Wajibu na Majukumu ............................................... 88
Kielelezo nambari cha 6.19: Kanuni za darasani kwa kazi ya kikundi ................ 89
Kielelezo nambari 6.20: Orodhahakiki ya kuendesha kazi ya kikundi yenye mafanikio .......................................................................................... 90
Kielelezo nambari 6.21: Mikakati ya kuweka katika vikundi kwa madhumuni mbalimbali ..................................................................................... 91
Kielelezo nambari 6.22: Utafautishaji wa usaidizi hatua kwa hatua.................. 94
Kielelezo nambari 6.23: Utafautishaji wa kujumuisha uwezo tafauti ................ 95
Kielelezo nambari 6.24: Mpango wa utafautishaji.......................................... 96
Kielelezo nambari 6.25: Video ya EENET'Siku ya mjumuisho', Programu ya 4 juu ya uandaaji wa masomo ............................................................... 97
Kielelezo nambari 6.26: Nakala ya video ....................................................... 98
Kielelezo nambari 6.27: Msaada kwa wanafunzi wenye ulemavu .................. 100
Kielelezo nambari 6.28: Kurekebisha vitendo vya wanafunzi wenye ulemavu 101
Kielelezo nambari 6.29: Hatua za kusaidia ujifunzaji ..................................... 102
Kielelezo nambari 6.30: Maoni muhimu........................................................ 103
Kielelezo nambari 6.31: Fanya na usifanye .................................................. 104
Kielelezo nambari 6.32: Kadi za maoni za igizodhima................................... 105
Kielelezo nambari 6.33: Maswali bora.......................................................... 106
Kielelezo nambari 6.34: Baadhi ya mikakati ya kuuliza maswali ..................... 107

Rejea ........................................................................................................ 109

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| EENET | Enabling Education Network |
| MECP-Z | Madrasa Early Childhood Programme – Zanzibar |
| NAD | Norwegian Association of Disabled |
| NFU | Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili- Norway |
| TEZ | Taasisi ya Elimu ya Zanzibar |
| UNICEF | United Nations International Children's Emergency Fund |
| WEMA | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali |

# Utangulizi

Moduli hii inampa mkufunzi njia za kubadilishana mikakati ya pamoja ya ufundishaji jumuishi ambao unakuza ujifunzaji mahiri wenye ufanisi katika mazingira mbalimbali, zikiwemo skuli ambazo hazina nyenzo za kutosha na zenye madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Mikakati hii imebuniwa ili kusaidia **utafautishaji** na ufanisi katika kupanga vikundi vyenye **uwezo mchanganyiko** katika kukuza mafanikio. **Utafautishaji** ni namna ambavyo mwalimu hupanga na kufikia mahitaji tafauti ya wanafunzi. Walimu hukidhi mahitaji tafauti ya ujifunzaji ya wanafunzi kwa kubadilisha maudhui yanayofundishwa, jinsi wanavyofundisha, na mbinu wanazotumia wanafunzi kujifunza.

Ujifunzaji mahiri unajumuisha wanafunzi kufikiria kile wanachokifanya. Katika aina hii ya ujifunzaji, wanafunzi hawawi wapokeaji tu. Ujifunzaji mahiri haujihusishi sana na upelekaji wa maarifa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi, badala yake unahusu ujuzi wa mwanafunzi wa kujifunza kwa kujitegemea. Ujifunzaji mahiri huwataka walimu kutumia kwa ustadi mikakati mbalimbali ili kuwashirikisha wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji. Hii hujumuisha uandaaji wa masomo, na shughuli shirikishi ili kuruhusu wanafunzi wenye uwezo tafauti kujifunza maudhui sawa, kutumia upimaji katika kusaidia ujifunzaji, na kurekebisha kazi ili kukidhi mahitaji ya kila mwanafunzi na mitindo yao ya ujifunzaji.

Mara nyingi walimu hukabiliwa na ukosefu wa nyenzo katika skuli zao, na kufundisha madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Matokeo yake, walimu huishia kutumia mbinu za mhadhara wakati wa ufundishaji. Jambo hili huwaacha wanafunzi kuwa wasikilizaji tu. Madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi ni changamoto mahsusi kufuatia ufunguaji upya wa skuli baada ya kuwa zimeshafungwa, mfano, baada ya majanga, maafa au vita. Vipindi vya mafunzo vilivyotolewa katika moduli hii huwasaidia walimu kukuza ujifunzaji mahiri kwa kiasi kikubwa, kwa madarasa yasiyo na nyenzo, yenye wanafunzi wenye uwezo tafauti, kuwawezesha wanafunzi wote kushiriki na kuinua kiwango cha ujifunzaji wao.

Mpango wa ufundishaji katika moduli hii lazima ufanywe kwa kurejea moduli za mafunzo mengine ya awali katika mfululizo huu. Moduli ya ziada juu ya ujumuishaji wa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada vilevile ni marejeo muhimu ambayo yanajumuisha ushauri na mwongozo katika kubaini mahitaji ya ziada na vidokezo vya vitendo na mawazo kwa walimu, ambayo yatawasaidiakwa

utafautishaji na kusaidia wanafunzi wenye mahitaji ya ziada katika mazingira ya skuli na darasani.

Kama ilivyokuwa katika moduli nyengine, mafunzo yaliyoelezewa hapa yanajikita kwenye matumizi ya njia shirikishi na mbinu za ujifunzaji mahiri zinazofuata kanuni hii ya msingi:

**“Ni lazima tutumie mbinu za mafunzo jumuishi ikiwa tunataka kuwafunza wengine kwa mafanikio jinsi ya kufundisha kwa mbinu jumuishi”.**

## Muda wa mafunzo

Mkufunzi anapaswa kurekebisha mafunzo haya kuendana na mazingira na muda uliopo kwa ajili ya mafunzo. Mkufunzi anaweza kuvitekeleza baadhi ya vitendo ikiwa muda hautoshi, au kuviongeza iwapo washiriki watahitaji usaidizi wa ziada wa kufahamu mada inayohusika. Ikiwa vitendo vyote vitatumiwa, kama ilivyopangwa, bila ya kuongeza au kupunguza vitendo, moduli hii itahitaji kiasi ya saa 12 15 za mafunzo kwa siku 2 na nusu hadi 3, kwa kutegemea urefu wa siku za mafunzo uliopendekezwa, muda wa mapumziko na mambo mengineyo.

# Kipindi cha 6.1: Ahadi yetu katika kuuendea mjumuisho

## Utangulizi

Kuwawezesha wanafunzi kuwa wachangamfu katika mchakato wa ujifunzaji ni mkakati muhimu sana kwa mjumuisho. Kipindi hiki cha kwanza kinakusudiwa kuwasaidia washiriki kutafakari kile wanachokijua au wanachofikiria wanakijua kuhusu elimu mjumuisho, na kitampa mkufunzi dalili ya maarifa waliyonayo au wasiyoyafahamu. Kipindi kitampa kila mshiriki fursa ya kukuza mikakati ya mbinu bora za ufundishaji kwa kuzingatia jinsi ya ufundishaji jumuishi unavyoonekana.

## Kitendo cha 6.1a: Mtazamo chanya wa mabadiliko

Kikuu

Muda: Dakika 20

**Maelekezo**

Kitendo hiki kinawapa washiriki fursa ya kuzingatia umuhimu wa kuwa na mtazamo makini ili kufanya kazi kwa ufanisi kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji wa wanafunzi.

Waeleze washiriki kwamba, wakati tunakubali mapungufu yaliyowekwa na sera na rasilimali za skuli, ili kuinua kiwango cha ujifunzaji tunahitaji kufikia madarasa jumuishi zaidi, na, ili kufanya hivyo, walimu wanatakiwa kuwa makini. Wanatakiwa kufikiri na kutenda kimjumuisho, kwa njia ya kirafiki kwa wanafunzi, na wanatakiwa kujitolea kuendelea kuimarisha.

Watake washiriki kufanya kazi katika vikundi. Ikiwezekana, vikundi hivi vinapaswa kuwa na mchanganyiko wa watu kutoka katika masomo tafauti na viwango tafauti vya uwajibikaji na uzoefu. Kipe kila kikundi nakala ya **Kielelezo nambari 6.1** na **Kielelezo nambari 6.2.**

**Kielelezo nambari 6.1** — **Majibu tendaji na na siyo tendaji**

**Kielelezo nambari 6.2** — **Taarifa tendaji na na isiyo tendaji**

Kitake kila kikundi kisome vielelezo vyote viwili. Baada ya kusoma **Kielelezo nambari 6.1 na 6.2,** kila kikundi kinahitaji kuamua ni taarifa gani kati ya **Kielelezo nambari 6.1 na cha 6.2** ni **tendaji** na zipi siyo tendaji**.** Waandike maelezo kwenye karatasi au waandike maelezo kando ya kipande cha karatasi tupu yenye safuwima mbili zenye vichwa vya habari - 'tendaji' na 'isiyo tendaji'.

Kitake kikundi kimoja kilete mrejesho juu ya walichokiamua na kisha wape washiriki nafasi ya kuelezea na kujadili maamuzi yao.

Kwa marejeleo ya mkufunzi, lugha ifuatayo inaweza kuonesha majibu yasiyo **tendaji:**

- "Hakuna nilichoweza kufanya";
- "Hivyo ndivyo nilivyo";
- "Ananitia wazimu sana";
- "Hawataruhusu hilo";
- "Nalazimika ku...";
- "Siwezi...";
- "Lazima...";

Lugha ifuatayo inaweza kuonesha majibu tendaji

- "Wacha tuangalie tunachoweza kufanya";
- "Naweza kubadilisha";
- "Nachagua...";
- "Nita...";
- "Ninajitolea kwa...";
- "Ninapendelea...";
- "Ninaweza...".

Elezea kwamba wote ambao ni 'watendaji'(proactive) huwa wanaelekeza nguvu zao kwenye mambo ambayo wanaweza kuyabadilisha, wakigundua kwamba uwezo wao wa kushawishi mabadiliko unaongezeka. Wale ambao 'sio watendaji'(reactive) huelekeza nguvu zao kwenye mambo ambayo wana wasiwasi nayo lakini hawana uwezo wakuyabadilisha. Sisitiza umuhimu wa washiriki kuwa 'watendaji' na kuwa na mitazamo chanya ya mabadiliko wakati

wa kupanga kuimarisha ujumuishaji. Hatimaye, eleza kwamba vitendo viwili vinavyofuata vinahusu kutafsiri mtazamo huu chanya katika maono ya jinsi wanavyotataka madarasa yao yawe yenye kuvutia.

## Kitendo cha 6.1b: Dira yetu, Malengo yetu

Kikuu

Muda: Dakika 40

**Maelekezo**

Kitendo hiki huwasaidia washiriki kukumbuka mafunzo yao kuhusu elimu mjumuisho na faida zake. Washiriki hutumia ufahamu huo kutambua maono jumuishi waliyonayo kwa wanafunzi wao ambayo wanaweza kuyafanyia kazi ili kufikia mafanikio.

Watake washiriki kurejea kwa muhtasari na kuelezea elimu mjumuisho ni nini. Nukta muhimu zinaweza kukusanywa kwenye chatimgeuzo au ubao.

Toa muhtasari wa nukta kuu, zilizoorodheshwa kutoka kwenye moduli ya 1, 'Utangulizi wa elimu mjumuisho'. Nukta hizi ni kama vile:

- Elimu mjumuisho inahusu kuongeza uwepo, ushiriki, na ufaulu wa wanafunzi **wote** katika skuli. Inajumuisha kurekebisha tamaduni, sera na matendo maskulini ili ziweze kukabiliana na tafauti za wanafunzi **wote** katika jamii.
- Elimu mjumuisho inajengwa juu ya ufahamu kwamba kutengwa kielimu hutokea kwasababu ya matatizo ya kimsingi katika mfumo wa elimu au skuli. Huwa haitoi nafasi ya kulaumu kwa kuwabagua wanafunzi kwa sifa au uwezo wao.
- Mbinu ya elimu mjumuisho huleta mabadiliko ili skuli ziweze kumkaribisha na kumuelimisha kila mwanafunzi kwa ufanisi.
- Elimu mjumuisho hushajihisha mabadiliko ya ufundishaji, ambayo husaidia ujifunzaji tafauti, kwa kutumia mbinu tafauti kuendana na mitindo tafauti ya ufundishaji.
- Elimu mjumuisho ni jambo ambalo tunaendelea kulifanyia kazi, kwasababu tunaweza kuendelea kuimarisha kila wakati.

Washiriki wafanye kazi kwa jozi au vikundi vidogovidogo. Lipe kila kundi **Kielelezo nambari 6.3** chenye mkusanyiko wa kadi za 'Dira yetu'.

## Kielelezo nambari 6.3 Kadi za ‘Dira yetu’

Wakaribishe washiriki kubainisha maelezo yoyote yanayowavutia, na hususan kwa yale yanayohitajika kwenye skuli zao. Baadae wachague maelezo ya dira moja ili kutoa lengo la madarasa yao wenyewe au skuli yote.



Mshiriki akisoma taarifa nchini Zanzibar

**[Maelezo ya picha: Mshiriki ameshikilia kipande kidogo cha karatasi chenye taarifa. Ni mikono yake tu ndiyo inayoonekana.]**

Kwa mfano, mshiriki ambaye ana mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni katika darasa lake, anaweza akavutiwa na kauli ya dira hii kutoka **Kielelezo nambari 6.3:**

‘Tuna matarajio makubwa kwa wanafunzi wote, wakiwemo wale wenye mahitaji ya ziada.’

Kwa hivyo mshiriki anaweza kuandika lengo lifuatalo:

*‘Nitarekebisha kazi ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi wangu mwenye ulemavu anaweza kushiriki katika kujifunza kikamilifu’.*

Mfano mwengine wa **Kielelezo nambari 6.3** wa maelezo ya dira ni:


‘Tunapanga shughuli kwa ajili ya kukuza mahusiano chanya miongoni mwa wanafunzi.’

Mshiriki ambaye anataka kuwapa wanafunzi majukumu zaidi, na anataka kuendeleza kazi ya kikundi, anaamua kuyafanyia kazi malengo yafuatayo:

‘Baadhi ya kazi za jozi au za kikundi zitafanyika katika masomo mengi, na kila mwanafunzi atapewa majukumu ndani ya kikundi ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anashiriki na anafanya kazi vizuri na kwa pamoja.’

Washiriki wataandika na kubadilishana malengo yao na kikundi jirani. Kisha waombe watu wa kujitolea kujadili lengo lao katika kikundi chote. Baadae malengo yanaweza kuoneshwa ukutani na kuangaliwa wakati wa mapumziko.

Ni muhimu kutoa mrejesho chanya na hususan kuidhinisha michango ambayo inakuza ushirikishwaji.



‘Dira yetu’ Maelezo kutoka kwa washiriki

**[Maelezo ya picha: Vipande 26 vya karatasi vyenye maandishi vimebandikwa ukutani kwa umbo la piramidi. Mwanamke amekaa upande wa kulia wa picha.]**

# Kitendo cha 6.1c: Kuelekea darasa jumuishi

Kikuu

Muda: Dakika 30

**Maelekezo**
Kitendo hiki huwasaidia washiriki kubaini vikwazo vinavyoweza kuondolew ili waweze kutimiza malengo yao ya mjumuisho kwa madarasa au skuli yao.

Mpatie kila Mshiriki Kielelezo nambari 6.4.

**Kielelezo nambari 6.4** **Kutambua malengo yetu**

Washiriki wafanye kazi mmojammoja na kuchagua lengo moja kutoka kwenye ukuta mwishoni mwa **Kitendo cha 6.1b.** Wachague lengo ambalo linaendana na darasa lao au mazingira ya skuli, na ambalo linawapa changamoto.

Mtake kila mshiriki kuzingatia mabadiliko ambayo anaweza kuhitaji kufanya kwenye matendo yao ili lengo hili lipate kufikiwa.

Baada ya washiriki kukamilisha **Kielelezo nambari 6.4,** watake washiriki wabadilishane majawabu yao katika jozi, kwa kuzingatia mawazo yoyote wanayotaka kuongeza au kubadilisha hoja walizotoa baada ya majadiliano yao. Kisha chagua baadhi ya washiriki au watake kujitolea, kuwasilisha mawazo yao kwa washiriki wote kwa ajili ya majadiliano na maoni zaidi.

# Kipindi cha 6.2: Kuandaa mazingira ya ujifunzaji mahiri

## Utangulizi

Lengo la moduli hii ni kukuza ujifunzaji mahiri na kufikia kwa kiwango kikubwa madarasa na skuli jumuishi. Jinsi darasa linavyopangwa linaweza kuwa na athari kubwa ikiwa kujifunza kwa vitendo kunaweza kupatikana na kama wanafunzi wanaweza kujiunga au kuzingatia masomo.

Katika kipindi hiki, washiriki wataona kwamba siku zote kuna jambo la kufanywa ili kuyafanya mazingira kuwa rafiki, jumuishi na tayari kwa ujifunzaji mahiri, hata pale ambapo madarasa yanaweza kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi au samani kidogo au duni.

## Kitendo cha 6.2a: Kutayarisha mazingira ya kujifunzia

Kikuu

Muda: Dakika 70

**Maelekezo**
Kitendo hiki kinawasaidia washiriki kufikiria njia za kuandaa mazingira ya kujifunzia ili kukuza ujifunzaji mahiri.

Sisitiza umuhimu wa kuandaa mazingira ya kujifunzia ambayo ni salama na yanayoweza kudhibitiwa kufundishia na kujifunzia, hata kama madarasa ni makubwa. Utayarishaji wa mazingira chanya ya kujifunzia unaweza kuleta tafauti kati ya darasa lenye utulivu, linalofanya kazi na lenye zogo.

**Kielelezo nambari 6.5** — **Picha za darasani**

**Kielelezo nambari 6.6** — **Majibu ya picha**

Washiriki wafanye kazi katika vikundi. Ikiwezekana wanapaswa kuwa mchanganyiko wa watu kutoka taaluma na viwango tafauti vya uwajibikaji na uzoefu.

Toa nakala ya **Kielelezo nambari 6.5** na **6.6.** Chenye maelekezo yafuatayo kwa kila kikundi:

- Angalia na jadili picha za madarasa katika **Kielelezo nambari 6.5**
- Angalia picha zilizoelekezwa kwenye kikundi chako na mkufunzi. Kikundi na 1 kiangalie picha nambari 1, Kikundi cha 2 kiangalia picha ya 2, na zaidi (Ikiwa kuna muda, vikundi vinaweza kuangalia na kujadili picha zaidi mara tu wanapomaliza kujadili picha yao ya kwanza).
- Fikiria maswali yafuatayo (Angalia **Kielelezo nambari 6.6**) na uandike baadhi ya maelezo:
  - Je! ni mambo gani mazuri kuhusu madarasa haya?
  - Je! ni changamoto au vikwazo gani vya kujifunza unavyoweza kuviona katika picha?
  - Je! ni wanafunzi gani wanaweza kutatizika katika mazingira haya ya kujifunzia na kwa nini?

Baada ya kiasi cha dakika 20, kitake kila kikundi waelezee kwa washriki wote walichojadili katika picha walizopewa.a. Vikundi vyengine vinaweza kuuliza maswali na kuongeza mawazo yao kuhusu picha hizo.



Kikundi kikiangalia na kujadili picha ya darasa

**[Maelezo ya picha: watu watatu wamekaa karibu ya meza, wakiangalia picha. Ni mikono yao tu iliyoshika kalamu ndio inayoonekana. Watu wawili wanaonesha kwenye picha kwa kalamu zao. Mtu aliye upande wa kushoto anaandika maelezo ya Kielelezo nambari 6.6]**

## Kielelezo nambari 6.7 — Mabadiliko yaliyopendekezwa

Baada ya takriban dakika 15 za majadiliano, gawa **Kielelezo nambari 6.7** na toa maelekezo yafuatayo kwa washiriki:


- Angalia tena picha zile zile (kikundi chako kinapaswa kuanza na picha waliyogaiwa mara ya mwisho).
- Jibu maswali kwenye **Kielelezo nambari 6.7**. Andika majawabu katika nafasi zilizoachwa chini ya maswali haya. Ikiwa unahitaji karatasi zaidi tafadhali omba:
  - Ni mabadiliko gani madogo unaweza kufanya katika madarasa haya ili kuhakikisha kuwa:
    - i. Wanafunzi wanajisikia salama na vizuri zaidi;
    - ii. Wanafunzi wanaweza kuona au kusikia vizuri zaidi;
    - iii. Wanafunzi na walimu wanaweza kuzunguka kwa urahisi zaidi.
  - Ni mabadiliko gani yanaweza kuhitajika ambayo hukuweza kufanya peke yako kama mwalimu? Elezea mabadiliko hayo.
  - Elezea nani mwengine anahitaji kuhusika na kwa nini.

Ruhusu kiasi cha dakika 20 kwa kazi ya kikundi. Wakati huo, onesha picha za darasani kutoka **Kielelezo nambari 6.5** zilizozunguka darasani.

Wakati vikundi vinapokuwa tayari, toa maelekezo haya:

- Kwenye kuta za darasa, kuna picha 6.
- Kata madokezo yako ya suluhisho na uyabandike chini ya picha zinazohusika. (Au yaandike kwenye maelezo ya baada yake)
- Kisha tembelea na uangalie kila picha na usome mapendekezo ya kila kikundi kwa ajili ya mabadiliko ya mazingira ya kujifunzia. Unaweza kuongeza mapendekezo yako mwenyewe na maoni kwenye picha kwa kutumia vikaratasi vidogo vya gundi vyenye maelezo (vikaratasi nata).

Baada ya kama dakika 10 za matembezi ukumbini watake washiriki wakae chini na kisha wabadilishane majawabu yao kwenye mabadiliko yaliyopendekezwa ambayo wameyasoma.




Mabadiliko yaliyopendekezwa na washiriki kwa mpangilio wa darasa

**[Maelezo ya picha: Picha ya darasa imebandikwa ukutani na jadweli la Kielelezo nambari 6.6. lenye maandishi limebandikwa chini ya picha. Vikaratasi vyenye gundi vilivyoandikwa mabadiliko yanayopendekezwa vimebandikwa juu yake na washiriki walioko karibu.]**

**Mazingatio kwa mkufunzi:**

Katika kisanduku hapa chini kuna majibu yanayowezekana kwa picha moja tu. Jukumu lako kama mkufunzi, unapaswa kufikiria kupitia majibu yanayowezekana kwa picha nyengine zote kabla ya kuendesha kipindi hiki. Badala yake unaweza kutumia picha kutoka kwenye skuli/mazingira yako mwenyewe, ilimradi tu unazingatia itifaki za ulinzi zilizowekwa kuhusu ushirikishaji wa picha za wanafunzi. Tafadhali kumbuka kwamba tafsiri zako za picha na zile za washiriki zinahitaji kuelezwa. Ikizingatiwa kuwa hutojua haswa kile kinachotokea kwenye picha, unatakiwa kuruhusu mitazamo tafauti ikiwa imethibitishwa/elezewa.

**Picha ya 1**

*Changamoto / Vikwazo*

- Kutokuwepo madeski/viti vya kutosha kwa kila mmoja.
  - Hiki kinaweza kuwa kikwazo kwa wanafunzi wenye matatizo ya utembeaji ambao wanaweza kupata ugumu wa kukaa sakafuni.
  - Pia ni kikwazo kwa mwanafunzi yeyote kwasababu ni vigumu kuzingatia masomo ikiwa atakua hana raha.
- Sakafu yenye vumbi
  - Wanafunzi pamoja na vitabu vyao huwa wanachafuka kwa sababu ya sakafu yenye vumbi.
  - Nguo chafu zinaweza kuwa kikwazo ikiwa wazazi/walezi wao wataudhika na kusema hawataki waende skuli wakichafuka hivyo. Au wanafunzi wenyewe wanaweza kuamua kuwa hawataki kukaa darasani ikiwa watalazimika kukaa katika sakafu chafu siku nzima. Kukaa kwenye sakafu inaweza ikawa baridi.
  - Mabuku machafu inawezekana ikawa ni vigumu kusoma au kuandika kwenye ukurasa ambao ni mchafu, jambo ambalo liwezekana likawa ni vigumu hasa kwa wanafunzi ambao hawaoni vizuri.
- Wanafunzi waliokaa kwenye madawati upande wa kushoto wa picha wanalazimika kugeuza miili yao ili waweze kuona ubao uliopo mbele ya darasa (ubao uliopo nyuma ya darasa labda ni ubao wa matangazo)
  - Hiki kinaweza kuwa kikwazo kwa mwanafunzi yeyote, kwani ni vigumu kujifunza na kuzingatia ikiwa hana raha.
  - Wanafunzi wenye matatizo ya kukumbuka au kuelewa wanaweza kupata ugumu wa kuzingatia ikiwa mara kwa mara watalazimika kuendelea kutembeza miili na vichwa kuangalia baina ya vitabu na deski lao na ubao.

*Mambo mazuri*

- Mng'ao, mwanga mzuri
- Inaonekana kuwa chumba kikubwa, chenye nafasi ya kutosha.
- Wanafunzi wanafanya kazi kwa vikundi

*Mabadiliko ambayo mwalimu anaweza kuyafanya ili kuondosha vikwazo hivi*

- Kwa uwangalifu panga ni nani atakaa katika dawati au sakafu. Kwa mfano wanafunzi ambao unaona ni vigumu kutembea, siku zote wanapaswa

wakae katika madawati. Kwa wanafunzi wengine watakaa kwa zamu, ili waweze kubadilishana kukaa katika dawati au sakafu.

- Unaweza kupanga shughuli ili vikundi vya wanafunzi wanaokaa juu ya madeski wafanye shughuli kwa kutumia vitabu na kuandika, na wale walio sakafuni wafanye shughuli nyengine zinazohusisha kufikiri, kuzungumza, kugusa au kutengeneza vitu. Baadae vikundi vinaweza kubadilishana.

- Unaweza kupanga upya madeski ili wanafunzi waweze kutembea kiasi kidogo ili kuona ubao. Unaweza hata ukabadilisha na likawa somo, kwa mfano, watake wanafunzi watengeneze miundo tafauti ya darasa ambayo wanadhani itawafaa zaidi. Wanaweza kubuni mipangilio ambayo itafanya kazi vizuri katika kazi za kikundi, kwa shughuli za kusikiliza, kufanya majaribio, na mengineyo. Baadae unaweza kujaribu miundo yao na kuwataka wanafunzi watathmini ni muundo upi unafanya kazi vizuri zaidi. Shughuli kama hii inaweza kuwasaidia kujifunza zaidi kuhusu upimaji, hesabati, kuchora na kubuni, vilevile kujifunza kufikiri kwa kina na hata ujuzi wa kuandika ripoti, kama utawataka waandike mchakato na matokeo waliyoyapata.

  Mabadiliko yanayohitaji msaada kutoka kwa wengine.
  Unaweza kuwashajiisha wanafunzi kuleta vipolo au mikeka kwa ajili ya kukalia, ikiwa wanakaa kwenye sakafu. Vipolo, busati na mikeka vinaweza kukung'utwa kwa urahisi, kutikiswa au kukoshwa na kukaushwa mara kwa mara. Hili linaweza kuhitaji usaidizi kutoka kwa wazazi/walezi, au wengine katika jamii ambao wanaweza kuchangia mikeka.

- Unatakiwa kutoa ndoo ya maji na sabuni ili wanafunzi waweze kuosha mikono yao baada ya kukaa kwenye sakafu. Hii itawasaidia wao kuwa salama na maambukizi na pia kuweka mabuku yao kuwa safi. Unaweza kuhitaji msaada kutoka kwa mtu mmojammoja kuchangia ndoo na sabuni ikiwa skuli haina pesa za kununulia.

- Unaweza kuwasiliana na wafanyabiashara wa ndani au jumuiya zisizo za kiserikali (NGOs) kushawishi kuchangia samani kwa ajili ya skuli yako. Wanafunzi katika darasa lako pia wanaweza kuhusishwa.

# Kitendo cha 6.2b: 'Muonekano wa darasa lililotayari kwa ujifunzaji mahiri'.

Kikuu

Muda: Dakika 30

**Maelekezo**
Shughuli hii inatoa mawazo ya vitendo kwa ajili ya kuandaa na kupanga nafasi ya kujifunza.

Kuna mambo mawili muhimu kwa mazingira ya darasa: Mazingira ambayo yanahusisha sehemu ya kuonekana, samani na nyenzo za darasani na saikolojia ya kijamii, ambayo yanahusisha maadili yaliyopo, tabia za darasani na jinsi inavoshughulikiwa, na jinsi wanafunzi na walimu walivyojisikia salama na kusaidiwa.

**Kielelezo 6.8** — **Kuandaa mazingira ya kuonekana darasani**

**Kielelezo nambari 6.9** — **Kuandaa mazingira ya saikolojia jamii ya darasani**

Andaa shughuli hii kabla ya kipindi. Nakili na kata kadi na zichanganye vizuri, kisha toa seti moja ya kadi kutokea ama **Kielelezo nambari 6.8** au **Kielelezo nambari 6.9** kwa kila kikundi. Hakikisha kuna takriban idadi ileile ya kikundi inayofanyakazi katika kila kielelezo. Vikundi 3 vinafanyia kazi **Kielelezo nambari 6.8** na vikundi 3 vinafanyia kazi **Kielelezo nambari 6.9.**

Kadi ziwe na 'kazi kuu iliopangwa' (Maandishi makubwa yaliyokozeshwa), na 'vitendo vya usaidizi ambavyo vitaweza kusaidia kutambua kazi hizo kuu za kuonekana na saikolojia jamii. Kadi zisaidie kuonesha jinsi darasa lililotayari kwa ujifunzaji mahiri unavotakiwa kuwa.

Katika vikundi washiriki wanapaswa kufikiria ni vitendo gani vya kusaidia vinavyoambatana na kazi kuu za uandaaji na kuweka kadi zinazohusika pamoja.

Katika **Kielelezo nambari 6.8** na **Kielelezo nambari 6.9** kadi zimepangwa kumuonesha mkufunzi majibu sahihi ili kurahisisha kuangalia kazi za vikundi.



Washiriki kutoka vikundi viwili wanajadili mawazo yao kuhusiana na kazi zilizopangwa na vitendo saidizi vya mazingira na saikolojia jamii.

**[Maelezo ya picha: wanawake saba wamekaa kuzunguka meza na wanaume watatu wamesimama. Wanaangalia vipande vidogovidogo vya karatasi vilivyopangwa kwa safu juu ya meza. Mwanamke mmoja anayeonesha moja ya vile vipande vya karatasi.]**

Baada ya dakika kumi vitake vikundi viwiliviwili viungane kuwa kikundi kimoja kilichofanya kazi katika **Kielelezo nambari 6.8** kiungane na kikundi kilichofanya kazi ya **Kielelezo nambari 6.9** (Moja kati ya vikundi hivyo wachukuwe kadi zao waelekee kwenye meza ya kundi jengine). Baadae wabadilishane fikra na mawazo yao kuhusu ‘kazi za kupanga’ kuhusu mazingira ya kuonekana na ya saikolojia ya jamii.

Wakiwa kikundi kizima watake wakupe mrejesho juu ya vitendo saidizi vilivyoambatanishwa kwa kila kazi kuu iliyopangwa.’Washiriki wajadili walichokiamua na athari ya zoezi lao la ufundishaji.

**Ukumbusho/zingatio kwa mkufunzi:**

Changamoto nyingi na mabadiliko yaliyojadiliwa katika **Kitendo cha 6.2a** vinaendana na washiriki wanaokabiliana na madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Kazi zilizopangwa na hatua za kusaidia zilizojadiliwa katika **Kitendo cha 6.2b**, hususan kinahusiana na changamoto zenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Ni muhimu kutambua hisia za mwalimu kwa madarasa yaliyozidiwa na idadi kubwa ya wanafunzi, na ni muhimu kiasi gani kwao kupanga kwa makini na kubuni mikakati ambayo itapunguza athari mbaya za madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi katika kujifunza.

Sisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wakufunzi wenzako na jamii kubwa zaidi katika kujaribu kuondosha changamoto za madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Pia ni muhimu kuwahusisha wanafunzi wenyewe. Ni muhimu sana kujenga hisia za kijamii ili kila mwanafunzi apate msaada anaohitaji ili kujifunza kwa mujibu wa uwezo wake.

Madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi yanahitaji ushirikiano na ujuzi wa kujitegemea kwa ustawi wa mazingira hayo. Ukuzaji wa ujuzi huu wa kujifunza ndio mkazo wa baadhi ya vitendo katika Moduli hii pamoja na Moduli ya 7: **Ukuzaji wa ushiriki wa mwanafunzi.**

Unaweza ukawa na uelewa wa miongozo mingi juu ya ufundishaji wa madarasa yenye wanafunzi wengi. Mmoja miongoni mwa miongozo muhimu ni Ofisi ya Elimu ya Kanda ya Asia na Pasifiki uliotolewa na UNESCO.

# Kipindi cha 6.3: Kukuza shughuli za kushajihisha ujifunzaji mahiri

## Utangulizi

Mikakati ya ujifunzaji mahiri huwawezesha wanafunzi kujishughulisha na kuwa hai katika mchakato wa ujifunzaji. Shughuli zinakuwa zinamshirikisha zaidi mwanafunzi, mara nyingi zinakuwa ni shirikishi, dadisi au hujikita kwenye tatizo na huhusisha uzoefu wa wanafunzi wa moja kwa moja.

Lengo la kipindi hiki ni kwa ajili ya washiriki kutambua umuhimu wa kutumia mikakati mbalimbali ya ufundishaji katika kila somo, na kupanga kwa ushirikiano fursa za ujifunzaji mahiri ambazo zitakuwa ni jumuishi na shirikishi.

## Kitendo cha 6.3a: Kutambua mikabala ya ujifunzaji mahiri

Kikuu

Muda:  Dakika 50

**Maelekezo**

Kitendo hiki kitawasaidia washiriki kuwa na uelewa wa baadhi ya mikakati ya ujifunzaji mahiri wanayoweza kuitumia, au tayari wanaitumia, katika madarasa yao.

Waulize washiriki wanafahamu nini juu ya 'ujifunzaji mahiri'. Baada ya kuandika mambo muhimu ya washiriki kwenye Chatimgeuzo au ubao, eleza kwamba kujifunza kwa vitendo kunatoa fursa kwa kila mmoja kuchangia na kujifunza.

Ikiwa vipengele hivi vikuu vitano havitafikiwa katika majibu ya washiriki, sisitiza kwamba ujifunzaji mahiri:

- **Unatoa fursa ya kusikiliza na kuzungumza:** Kuzungumza ni msingi wa mchakato wa kuelezea, kujifunza na kufahamu;
- **Ni shirikishi:** wanafunzi wanafanya kazi na kuendelea pamoja;
- **Shajihishi**: wanafunzi wanapata fursa na shauku ya kushiriki kikamilifu;
- **Inachochea fikra**: msisitizo upo kwenye kuuliza, kutatua matatizo na kuongeza taaluma;

- **Inabadilika**: inavutia na kufundisha mitindo tafauti ya kujifunzia.

| | |
|---|---|
| **Kielelezo nambari 6.10** | **Video ya EENET ya 'Siku ya Mjumuisho', mpango wa 7 kuhusu ufundishaji na ujifunzaji** |
| **Kielelezo nambari 6.11** | **Dondoo muhimu kutoka kwenye nakala za video** |
| **Kielelezo nambari 6.12** | **Mbinu za ujifunzaji kwa vitendo** |

Kufuatia maoni hayo, washiriki wanapaswa kutazama kipindi cha 7 kutoka kwenye kifurushi cha mafunzo ya video cha EENET 'siku ya mjumuisho', ambacho kinalenga ufundishaji na ujifunzaji (**Kielelezo nambari 6.10**). Kama huwezi kupata video mtandaoni, kipe kila kikundi nakala za video[1] (**Kielelezo nambari 6.11**)

Sasa mpe kila mshiriki **Kielelezo nambari 6.12** chenye maelekezo yafuatayo:

- Tazama video kwenye **(Kielelzo nambari 6.10)** au angalia dondoo za **(Kilelezo nambari 6.11).** Video hii inatoa mawazo ya jinsi ya kuyafanya masomo kuwa yanamshirikisha mwanafunzi zaidi.
- Wakati wanaangalia video, tumia **Kielelezo nambari 6.12** kutengeneza orodha ya mbinu zote za ujifunzaji mahiri kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kushiriki na kufikia yale ulioyaona katika video au kuyasoma katika nakala. Tafuta vitendo, nyenzo na mikakati iliyotumiwa.
- Jadili katika vikundi vyenu:
  - Mbinu gani ambazo hamzifahamu na mnataka kuziingiza katika mpango kazi wenu?
  - Je kuna mikakati myengine yoyote ya ujifunzaji mahiri jumuishi tungeweza kuitumia katika hali hizo ambayo haikuoneshwa katika video?

Baada ya dakika 10 za majadiliano ya kikundi andika ubaoni au kwenye chatimgeuzo nukuu muhimu walizotoa washiriki. Unganisha mjadala kwenye **vipengele 5 vikuu vya ujifunzaji mahiri** zilizotajwa hapo juu: kuzungumza na kusikiliza, kushirikiana, kuhamasisha, kuchochea mawazo na aina nyengine mbalimbali.

Mazingatio kwa mkufunzi:
Angalia kisanduku cha hapa chini chenye orodha ya mbinu za ujifunzaji mahiri zilizooneshwa au kutajwa katika video.

Orodha ya mbinu zinazoonekana au zilizotajwa kwenye video:

- Shughuli zinazohusisha kutizama au kuangalia.
- Shughuli zinazohusisha kusikiliza na kufahamu.
- Shughuli zinazohusisha mazungumzo
- Shughuli zinazohusisha kugusa vitu
- Shughuli zinazohusisha mwendo
- Kutumia michezo
- Kutumia midoli;
- Kufanya masomo yaendane na uzoefu wa maisha halisi;
- Kutumia maisha halisi na vitu vinavyocha katika;
- Kutumia ujifunzaji unaojikita katika miradi
- Kutumia igizodhima, tamthilia na utendaji;
- Kutumia nafasi za nje;
- Kutumia kazi ya vikundi;
- Kutumia kazi ya jozi;
- Kutumia ujifunzaji rika na rafiki au mfumo rika saidizi;
- Kutumia vitabu vya kiada kwa njia ya ubunifu.

## Kitendo cha 6.3b: Upangaji wa shughuli zinazokuza ujifunzaji mahiri

Kikuu

Muda: Dakika 60

**Maelekezo**
Kitendo hiki kimeandaliwa kusaidia washiriki kukuza uthubutu wao kwenye kupanga vitendo vinavyoshirikisha, kujumuisha na kukuza ujifunzaji mahiri. Kitendo hiki kitawapa washiriki fursa ya kupanga kwa pamoja kiubunifu baadhi ya vitendo vya masomo ambavyo vitakua jumuishi.

Kwanza, sisitiza haja ya kuandaa andalio la somo kwa uangalifu. Wakati ukitambua kwamba washiriki mara nyingi wanaweza kutegemea vitabu vya kiada pekee, ni muhimu kwamba somo liandaliwe kutokana na malengo ya kujifunza ambayo yanajengwa juu ya maarifa ya kile ambacho mwanafunzi anahitaji kujifunza baadae. Hata kama washiriki wataendelea kutumia vitabu vya kiada, wanahitaji kujitayarisha kwa umakini jinsi wanavyowasilisha somo ili wanafunzi wafahamu kilichoandikwa.

Sisitiza jinsi ya upangaji mzuri wa somo utakavyomsaidia mwalimu kujiamini darasani. Watajua mapema cha kufanya na watajipa muda kutayarisha nyenzo za kujifunzia ambazo zinaongeza ushiriki wa wanafunzi. Hii ina umuhimu wa kipekee hasa kwa madarasa yenye wanafunzi wengi. Kwa malengo yaliyowazi ya somo, washiriki wanaweza kutayarisha na kukabili vitendo ili kuhakikisha maendeleo ya wanafunzi ili kufikia malengo hayo. **Kwa mafanikio ya somo, walimu wanatakiwa wawe wazi na wafahamu vizuri wanachokifundisha,** na wanafunzi watambue wanachotarajiwa kujifunza.

Mwisho, fahamu kwamba andalio la somo litakua na ufanisi zaidi ikiwa walimu watafanya kazi kwa pamoja. Wanaweza kusaidiana kutatua matatizo na kupanga masomo mjumuisho yenye kuvutia zaidi, ikiwa watabadilishana mawazo na uzowefu.

**Kielelezo nambari 6.13** **Malengo ya ujifunzaji**

Washiriki wafanye kazi katika vikundi. Wakumbushe kuhusu mbinu na mikakati ya ufundishaji ambayo waliyoibainisha kwenye **Kitendo cha 6.3a.** Kipe kila kikundi kadi tafauti zilizokatwa kutoka **Kielelezo nambari 6.13.**

Kila kikundi kiangalie kadi yao ya lengo la ujifunzaji. Wakifanya kazi kama kikundi wanalazimika kuandaa kitendo kimoja cha ujifunzaji ambacho kitachochea ujifunzaji mahiri na kinaweza kuwasaidia wanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji.

Itakua ni msaada kwao kuwapa mfano wa jinsi ya kufanya hili. Chagua moja ya malengo ya ujifunzaji, kwa mfano, lengo la ujifunzaji wa hisabati. Kisha watake washiriki wajipange katika safu kwa mujibu wa urefu wao. Elezea kwamba kitendo hiki kinaweza kutumiwa kufafanua istilahi kuanzia ndogo kwenda kubwa "Ascending" na kuanzia kubwa kuja ndogo "Decending". Huu ni mfano wa kitendo kimoja ambacho kinakuza ujifunzaji mahiri na kinawawezesha

wanafunzi kuendelea kufikia lengo la ujifunzaji wa lengo la hisabati lililopo kwenye kadi. (Ni muhimu kukiambia kikundi chenye kadi hii wasitumie kitendo kile kile).



Washiriki wanaonesha shughuli ya ujifunzaji wa hisabati Zanzibar

**[Maelezo ya picha: Mwanawake mmoja amesimama na wanne wamekaa karibu na meza wakinyanyua michoro inayoonesha sehemu za ukubwa tafauti.]**

Baada ya dakika 20 (Au mara tu, ikiwa kila mmoja amemaliza), kila kikundi kitafanya mrejesho wa kitendo walichokifanya. Kikundi chote kinaweza kikajadili kama kitendo kinakuza ujifunzaji mahiri na kinasaidia kufikia lengo la ujifunzaji.



Kujadili kitendo cha ujifunzaji wa somo la sayansi wakati wa matembezi ukumbini Zanzibar

**[Maelezo ya picha: Mwanamke amesimama karibu na ukuta.  Kwa kutumia fimbo anaonesha katika vipande viwili vya Chatimgeuzo vilivyogandishwa ukutani. Vipande hivyo vimeandikwa habari zinazohusu ujifunzaji mahiri wa somo la sayansi kuhusu mimea.]**

**Kielelezo nambari  6.14** **Mikakati ya ujifunzaji mahiri**

Wape washiriki **Kielelezo nambari 6.14** na kitake kila kikundi kitafute mkakati uliomo katika orodha inayoelezea kitendo chao. Kisha kila kikundi kitengeneze kitendo zaidi ambacho kitapelekea ujifunzaji mahiri na kitasaidia wanafunzi kufikia lengo lao la ujifunzaji.  Watapitia orodha yao ya mawazo katika kufanya hilo.

Vitendo walivyovifanya viandikwe kwenye Chatimgeuzo na vioneshwe kwenye kadi zao zenye lengo la ujifunzaji kutoka kwenye **Kielelezo nambari 6.13.** Onesho linahitaji kuhifadhiwa kwa uangalifu na kuoneshwa tena wakati wa **Kitendo cha 6.5c.**

**Zingatio kwa mkufunzi:**
Wakati wa mjadala wa mrejesho wa hapo juu, kipe kila kikundi changamoto ya kuelezea vipi vitendo walivyovibuni vinaweza kufikiwa na wanafunzi wenye mahitaji ya ziada, kama vile kuwa na mahitaji maalumu ya kielimu kwa watu wenye ulemavu. Upangaji kwa ajili ya kuwajumuisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada ni sehemu muhimu ya upangaji wa somo la Elimu Mjumuisho.

Hii itashughulikiwa zaidi katika vipindi vifuatavyo.

# Kipindi cha 6.4: Kupanga na kuendesha kazi ya kikundi

## Utangulizi

Wanafunzi hujifunza kwa kiasi kikubwa kwa kuelezea mawazo yao kwa wenzao na kushiriki katika vitendo ambavyo wanaweza kujifunza kutoka kwa wanafunzi wa rika zao. Hukuza ujuzi wao katika uandaaji na upangaji wa vitendo vya ujifunzaji, hufanya kazi kwa ushirikiano, hutoa na kupokea mrejesho na hutathmini ujifunzaji wao.

Lengo la kipindi hiki ni kujenga uthubutu wa washiriki kupitia mazoezi ya upangaji na uendeshaji wa kazi za kikundi na jozi.

## Kitendo 6.4a: Kwa nini kazi ya kikundi ni muhimu?

Kikuu

Muda: Dakika 40

**Maelekezo**
Washiriki wataona faida za kazi za kikundi na jozi na jinsi zinavyokuza ujifunzaji, na kuzingatia njia za kutatua changamoto za uendeshaji wa kazi ya kikundi kwenye madarasa yenye wanafunzi wengi.

Elezea kuwa kazi ya kikundi ni mkakati muhimu sana kwa mjumuisho na watake washiriki kukumbuka video ya EENET kwenye **Kielelezo nambari 6.10** iliyotumika katika **Kitendo cha 6.3a** kilichopita. Onesha tena sehemu ya video **(Baina dakika 8:49 na 9:53)** au andika toleo lililofupishwa na nakala (Lililotolewa hapo chini) kwenye Chatimgeuzo au ubao:

"Kazi ya kikundi inamaanisha kwamba watoto wanafanya kazi pamoja kubadilishana mawazo yao ili kufanya jambo zuri…… pia inaruhusu watoto kukubaliana…. na watoto wazito wa kufahamu kufanya vizuri zaidi. Kazi ya kikundi inatoa furaha kwa watoto na mwalimu wao, kiukweli, hufurahi kuwaangalia watoto wanaendelea na wanapata kitu fulani… Watoto wanahitaji kuwa wachangamfu na kuwa na mwalimu wao. Jukumu letu ni kuwaongoza katika kazi zao. Wao ndio watendaji wakubwa katika elimu yao". Mwalimu Honorine Boussini.

Wakumbushe washiriki kwamba kazi nyingi ambazo wamezifanya katika mafunzo haya zimefanywa kwa vikundi.


Kitake kila kikundi kijigawe katika vikundi vidogovidogo viwili au jozi mbili. Moja kati ya vikundi vidogo viwili au jozi kutoka kila kikundi kijadili **faida** za kazi ya kikundi na jozi darasani, ikiwemo darasa lenye wanafunzi wengi, kinyume na wanafunzi kufanya kazi wenyewe binafsi. Wanaweza kushajihishwa kurejea uzoefu wao wa kufanya kazi za kikundi na vipi kazi za kikundi zimewasaidia katika kipindi cha warsha hizi.

Washiriki waorodheshe mambo makuu kutoka katika mijadala yao. Unaweza kutoa baadhi ya mifano, kama vile 'akili za watu wawili ni bora kuliko ya mtu mmoja' 'Mawazo zaidi yalipatikana'.

Kikundi kidogo chengine huzingatia baadhi ya changamoto za kufanya kazi za kikundi, hasa katika madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Mifano inaweza kujumuisha 'Hakuna nafasi ya kusogeza viti na madawati' 'Kelele zinazoingilia madarasa mengine'. Kwa mara nyengine tena wanaorodhesha changamoto hizo.

Baada ya kama dakika 5, kila kikundi/jozi kitajiunga na kikundi/jozi nyengine kutoka kwenye kikundi chao na kubadilishana mawazo, kujadili na kulinganisha faida na changamoto walizobainisha.

Baada ya kama dakika 10, pokea mrejesho kwa ufupi kutoka kwa baadhi ya vikundi, bainisha masuala yoyote maalumu au tafauti yanayoibuka na toa picha ya muelekeo wa faida na changamoto zilizobainishwa. Haya yataorodheshwa katika Chatimgeuzo au ubao.



Chatimgeuzo zilizoorodhesha faida na changamoto za kazi ya kikundi

**[Maelezo ya picha: Karatasi mbili za Chatimgeuzo zimebandikwa ukutani. Moja ina mada ya 'faida' na nyengine ina mada ya 'changamoto'. Karatasi zote mbili zimebeba taarifa nyingi zilizoandikwa.]**

## Kielelezo nambari 6.15 — Faida na changamoto za kazi ya kikundi

Wape **Kielelezo nambari 6.15** kila kikundi. Watake washiriki wasome kwa pamoja orodha
ya faida na changamoto, wakijadili kila kilichokuwa kipya kwao,

Mwisho, vishajihishe vikundi kutoa mawazo kuhusu vipi wanaweza kuzitatua changamoto zilizobainishwa ili kazi ya kikundi iweze kufanywa kwa ufanisi. Kila kikundi kinaweza kikapewa changamoto mbili au tatu na kupewa dakika chache kutoa suluhisho. Baadae haya yanarejeshwa kwenye kikundi kwa ajili ya mjadala zaidi.

## Kitendo cha 6.4b: Kupanga kazi za kikundi

Kikuu

Muda: Dakika 30

**Maelekezo**
Kitendo hiki huwasaidia washiriki kupanga na kusimamia kazi ya kikundi kwa ufanisi, ikiwemo madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Wasisitize washiriki kwamba ufundishaji fanisi huchanganya ufundishaji wa darasa zima, mwanafunzi mmommoja, jozi na kazi ya kikundi wakati wa kila somo ili kuongeza utayari, ushiriki na ujifunzaji. Kwahivyo, ni muhimu walimu wajue ni wakati gani watatumia kikundi, na wataandaa kwa umakini kuhakikisha athari bora zaidi.

Eleza kwamba mara nyingi, unaposhauriana na wanafunzi kuhusu nani wanaweza kufanya kazi nao vizuri, walimu wataamua muundo wa kila kikundi kuliko kuwaacha wanafunzi kuamua wenyewe. Walimu wataamua muundo wa makundi tafauti kwa madhumuni tafauti. Hii ni muhimu kwa sababu inaruhusu mazingira tafauti zaidi ya kujifunza na itawashajihisha wanafunzi wote kushiriki kikamilifu.

Kwenye chatimgeuzo au ubao, onesha ni vipi mbinu tafauti za utengenezaji wa vikundi na mikakati inaweza kutumika kwa madhumuni tafauti katika viwango vya wanafunzi wenye uwezo tafauti darasani.

Mbinu hizi ni pamoja na:

- **Vikundi vyenye uwezo tafauti** ambapo wanafunzi wenye ujuzi tafauti, maarifa na uwezo wanaweza kukaa pamoja kwa kutatua matatizo;
- **Vikundi lengwa** ambapo wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaweza kupokea ufundishaji makini unaozingatia mahitaji yao;
- **Vikundi vyenye uwezo sawa;** mwalimu anaweza kupanga kazi katika kiwango chao au kuwacha vikundi vya wanafunzi wenye kasi zaidi kuendelea na kazi ili msaada wa ziada uweze kutolewa kwa wanafunzi wengine.

Ongoza kuwapanga wanafunzi katika **jozi** kuna faida nyingi za kazi ya kikundi lakini wakati mwengine kunaweza kutumika kudumisha kasi ya somo, kwa kuepuka muda unaotumika ‘kuingia katika vikundi’. Kufanya kazi katika jozi kunaweza pia kuhakikisha kuwa kila mmoja anahusishwa, kwani ni vigumu sana kwa wanafunzi katika jozi kuepuka kushiriki. Zaidi ya hayo, kazi ya jozi inaweza

kutumika wakati hakuna nafasi kwa vikundi kufanya kazi au kwa mwalimu kusimamia.

Katika kitendo hiki washiriki wanazingatia jinsi wanavyoweza kupanga vyema kujifunza kufundisha kazi maalum.

**Kielelezo nambari 6.16.** **Kupanga muundo wa kila kikundi**

Washiriki wafanye kazi kwa vikundi. Kipe kila kikundi seti ya kadi zilizokatwa kutoka kwenye **Kielelezo nambari 6.16.** Ni lazima waamue kama kazi inafanywa katika vikundi vya wanafunzi wenye uwezo tafauti, vikundi lengwa au vikundi vyenye uwezo sawa. Ni lazima pia waamue ni lengo lipi ('Kwanini'?) kadi ('katika mlazo') inaunga mkono uwamuzi wao.



Kikundi kinachofanya kazi ya kadi ya 'utungaji wa kikundi'

**[Maelezo ya picha: wanaume wawili na wanawake watano wamekaa katika viti huku wakiwaangalia wanawake wawili waliokaa sakafuni wakiandika kazi ya kadi ya "utungaji wa kikundi" kupitia majadiliano ya pamoja.**]

Hatimaye, washiriki watumie kadi tatu tupu kuunda kazi yao wenyewe, ili kutambua ni aina gani ya mkusanyiko utafaa zaidi, na waelezee ni kwa nini, Mawazo haya yanaweza kuchangiwa na kikundi kizima.

Katika kadi kwenye **Kielelezo nambari 6.16** zimepangwa ili kuonesha majibu sahihi ya kumsaidia mkufunzi kuangalia kazi za vikundi.

Elezea kwamba ushahidi wa utafiti juu ya athari za mazoea ya kupanga wanafunzi unaopendekeza kuwa hakuna muundo mmoja wa kugawa vikundi unaowanufaisha wanafunzi wote kwa wakati wote. Muhimu ni kwamba walimu wapange vikundi vya kujifunzia kwa haki ili wanafunzi maalumu, wakiwemo wasichana na wanafunzi wenye mahitaji ya ziada, wasiwakilishwe kupita kiasi kwenye vikundi vinavofanya vibaya. Kutumia vikundi vya watu vyenye uwezo tafauti darasani kunamaanisha kuwa wanafunzi wenye uwezo zaidi wanaweza kuimarisha ujifunzaji wao kwa kuwasaidia wengine, na wanafunzi wasio na uwezo wanaweza kufaidika kutokana na kufanya kazi kwa pamoja na wanafunzi waliojishughulisha zaidi na wenye ari.

**Kielelezo nambari 6.17** **Orodhahakiki ya kupanga kazi ya kikundi iliyobora**

Mpe kila mshiriki **Kielelezo nambari 6.17** na watake wajadili orodhahakiki kwa jozi. Kisha wabainishe mapungufu yoyote na kuamua kama ni chombo muhimu cha kuwasaidia walimu kupanga kwa ajili ya kazi za kikundi. Waombe washiriki wazingatie kama kuna mahitaji yoyote zaidi yanayohitajika kutambuliwa kwa ajili ya kupanga kazi ya kikundi katika madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi.

## Kitendo cha 6.4c: Kuendesha kazi za kikundi

**Kikuu**

Muda: Dakika 40

**Maelekezo**
Kitendo hiki kitawasaidia washiriki kuendesha kazi ya kikundi darasani kwa mafanikio.

Sisitiza umuhimu wa kuweka kanuni za kazi ya kikundi darasani. Ili kazi ya kikundi ifanikiwe, wanafunzi wote wanatakiwa kushirikishwa katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa uwajibikaji na mwalimu anatakiwa kutayarisha njia zake kuhakikisha haya yanakuwa mazoea.

Washiriki hufanyakazi kwa vikundi.

**Kielelezo nambari 6.18** **Wajibu na Majukumu**

Kata na toa seti ya kadi zilizotengenezwa kutoka katika **Kielelezo nambari 6.18** kwa kila kikundi.

Kila seti ya kadi inajumuisha:

- 'Kadi nne za jukumu' – mwenyekiti, mtunza kumbukumbu, mwandishi, mratibu na mtunzamuda.
- Kadi nne zinazoelezea majukumu;
- Kadi za mifano ya mambo ambayo watu wanaweza kusema katika majukumu yao (Kwa hati mlalo)

Kitake kila kikundi kuamua ni kadi gani ya maelezo ya jukumu inaendana na kadi za jukumu gani. Kisha wanahitaji kuamua ni kadi gani kati ya 'kile ambacho watu wanaweza kusema kinaendana na jukumu gani. Washiriki wanaweza kuandika kwenye kadi tupu za ziada kutoa mifano zaidi ya kile ambacho wanafunzi wanaweza kukisema katika majukumu hayo.

Kadi kwenye **Kielelezo nambari 6.18** zimepangwa ili kuonesha majibu sahihi ili kumsaidia mkufunzi kuangalia kazi za vikundi.

Kisha waombe washiriki wabungue bongo na kuja na orodha ya kanuni ambazo wanafunzi wanapaswa kufuata ili kazi ya kikundi iendeshwe kwa mafanikio. Hizi zinaweza kuandikwa kwenye chatimgeuzo au ubao.




Washiriki wakipanga kadi za majukumu ya kazi za kikundi

**[Maelezo ya picha: Vipande vidogo vya karatasi vyenye maandishi vimepangwa kwenye jadweli katika muundo wa mraba fito (gridi) na mikono mitano imeshika/ inaweka vipande vya karatasi.]**

**Kielelezo nambari 6.19** — **Kanuni za darasani kwa kazi za vikundi**

Kipe kila kikundi **Kielelezo nambari 6.19** ili walinganishe na bunguabongo la kikundi kizima. Wanaweza kuandika katika kadi tupu za ziada ili kutoa mifano zaidi ya kanuni muhimu.

Kisha kikundi kizima kijadili jinsi wanavyoweza kutumia moja kati ya vielelezo viwili hivi **(6.18 na 6.18)** ili kuwafunza wanafunzi katika skuli zao. Wanaweza kupendekeza njia zaidi ya kuwasaidia wanafunzi ili kujifunza jinsi ya kufanya kazi vizuri katika vikundi. Hii inaweza kujumuisha wanafunzi kuhusishwa katika kuunda kanuni wao wenyewe, au kutengeneza mabango na kutangaza zoezi la kazi nzuri ya kikundi.

**Kielelezo nambari 6.20** — **Orodhahakiki ya kufanya kazi bora ya kikundi**

Mpe kila mshiriki **Kielelezo nambari 6.20** na watake wajadili orodha hakiki wakiwa kwenye jozi. Wayaainishe mapungufu yote na kuamua kama ni zana muhimu ya kuwasaidia walimu kuendesha kazi za vikundi.

Kisha watake washiriki kukumbuka aina ya vitendo vya kikundi walivyovifanya wakati wa warsha za mafunzo hadi sasa.

**Kielelezo nambari 6.21** — **Mikakati ya kuweka vikundi kwa madhumuni tafauti**

Hatimaye, toa **Kielelezo nambari 6.21** kama kitini ili washiriki wakisome na kukihifadhi kwa ajili ya marejeleo ya siku zijazo kama mfano wa baadhi ya mikakati ya kuunda vikundi. Nyenzo hii inatoa mifano ya mikakati ya kuunda vikundi inayotumika kwa madhumuni maalumu.

Ikiwa kuna muda, kikundi kijadili kielelezo hiki ili kufahamu kila mkakati. Washiriki wanaweza kufikiria mifano ya darasani ya jinsi ya kutumia kila mkakati wa kuunda vikundi (mfano, fikiria tatizo/swala ambalo linaweza kutatulia kwa kutumia mbinu ya 'fikiri', jozisha 'shirikisha').

# Kipindi cha 6.5: Tumia utafautishaji katika madarasa yenye wanafunzi wenye uwezo tafauti

## Utangulizi

Andika nukuu hii yenye nguvu ubaoni au Chatimgeuzo ili washiriki waisome mwanzo wa kipindi hiki:

"Wito wangu katika maisha ni kuhakikisha kwamba kila mtoto anafikia uwezo wake kamili, kwamba ninafungua uwezo huo, kwamba chochote kile anachohitaji kufikia ninafanya hivyo."

Kujifunza kwa vitendo kunahitaji walimu kuwashirikisha wanafunzi wenye uwezo tafauti katika mchakato wa kujifunza. Kwa kutumia mbinu ya utafautishaji, mwalimu arekebishe mbinu za ufundishaji, mikakati ya ufundishaji na tathmini, na maudhui ya mtaala ili kuhamasisha na kumuwezesha kila mwanafunzi binafsi aweze kupata mafanikio ya kujifunza na kupata uzoefu (Angalia Moduli ya ziada ya **kujumuisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada** kwa vidokezo zaidi vya kuhamasisha na kuwezesha wanafunzi wenye mahitaji tafauti).

Mbinu mbalimbali za utafautishaji tayari zimerejelewa katika moduli za awali, kwa mfano, jinsi ya kurekebisha visaidizi vya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi mahitaji ya mwanafunzi mmojammoja katika moduli ya 5. Vipindi vya awali vya moduli hii pia vilichunguza mbinu za utafautishaji, ikijumuisha mikakati ya kujifunza kwa vitendo katika **Kipindi cha 6.3** na kupanga upatikanaji wa kujifunza kupitia kazi za kikundi au jozi katika **Kipindi cha 6.4.**

Walimu bora huhakikisha kwamba wanafunzi wote katika madarasa yao wanashiriki na kufaulu. Wanajua kwamba wanafunzi wote hujifunza tafauti na wanaweza kuhitaji aina tafauti za usaidizi.

## Kitendo cha 6.5a: Kuanzisha utafautishaji

Kikuu

Muda: Dakika 20

**Maelekezo**
Kitendo hiki kinawawezesha washiriki kufahamu maana ya 'kutafautisha'.

Waulize washiriki wanafahamu nini kuhusu 'kutafautisha'. Wahimize kufikiria juu ya kile ambacho tayari wanafanya darasani na kile ambacho kimeshughulikiwa katika vipindi vya awali. Andika mapendekezo kutoka kwa washiriki ubaoni au kwenye Chatimgeuzo.

Kufuatia hili fanya mambo haya:

- Utafautishaji unamaanisha kufundisha maudhui yaleyale lakini kwa njia tafauti ili wanafunzi wote kufikia lengo la kujifunza.
- Kuna mikakati ya pamoja ambayo inaweza kutumika. Mikakati hii inaweza kuwa na ufanisi katika madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi na yenye wanafunzi wa umri na uwezo tafauti.
- Ujifunzaji wa ushirikiano na warika (ambazo zilirejelewa katika **Kipindi cha 6.4)** ni njia ya kutafautisha, kama ilivyo mikakati mengineyo ya ujifunzaji mahiri ambayo tayari imeshughulikiwa katika moduli hii (k.m. katika **Kipindi cha 6.3)**
- Kuwajua wanafunzi wako ni hatua ya kwanza muhimu ya kutafautisha. Walimu wanahitaji kujua kiwango cha kila mwanafunzi, wanachopendelea na maslahi yao ya kujifunza, asili, uwezo na mahitaji (kipindi kijacho katika moduli hii, **Kipindi cha 6.6,** kitaangalia tathmini kwa undani).

Tumia mapendekezo kutoka kwa washiriki kwa vipengele vitatu vya ufundishaji:

- Maudhui;
- Jinsi maudhui yanavyofundishwa;
- Jinsi maudhui yanavyo tathminiwa.

Sisitiza mapendekezo yoyote kutoka kwa washiriki yanayounganisha utafautishaji kwenye ujumuishi wa wanafunzi wa uwezo tafauti kwa kurekebisha ufundishaji ili kukidhi mahitaji ya mtu binafsi. Lengo kuu la kipindi hiki ni kutambua jinsi maudhui yanavyofundishwa. Pia kipindi kitawasaidia washiriki kubuni na kurekebisha vitendo na vifaa ili kuhakikisha ushirikishwaji wa wanafunzi wenye uwezo na mahitaji mbalimbali.

Iwapo washiriki wanaifahamu vyema dhana ‘kusaidia hatua kwa hatua’ (scaffolding) kama mkakati wa kusaidia ujifunzaji, eleza kile kinachofahamika kwa istilahi kusaidia hatua kwa hatua (scaffolding) na jinsi linavyotafautiana na ‘utafautishaji’:

- Kwa ujumla, ‘kusaidia hatua kwa hatua’ ni istilahi inayotumiwa kuelezea muongozo binafsi, msaada, na usaidizi ambao mwalimu au wanafunzi wa rika moja hutoa kwa mwanafunzi, na jinsi mwalimu anavyounda maudhui ya somo ili lengo la kujifunza liweze kufikiwa hatua kwa hatua na darasa zima-kama vile kugawanya mafunzo katika vipande vinavyoweza kudhibitiwa na kisha kutoa zana au muundo kwa kila kimoja. Kwa mfano, wakati wa kusoma matini, mwalimu anaweza kuhakiki maandishi na kujadili msamiati muhimu, au kusoma maandishi vipandevipande na kuyajadili wakati wanapoyasoma.
- Kwa kutumia utafautishaji, hata hivyo, mwalimu anaweza kumpa mwanafunzi matini tafauti zilizofupishwa au zilizorekebishwa na/au kurekebisha zoezi linalofuata kwa wanafunzi tafauti.

**Mazingatio kwa mkufunzi:**
Iwapo mkufunzi anahisi kuna haja ya kueleza zaidi tafauti kati ya ‘kusaidia hatua kwa hatua’ na ‘utafautishaji’ kisha washiriki wanaweza kufanya vitendo kwa dakika kumi zifuatazo.

**Kielelezo nambari 6.22** **Usaidizi hatua kwa hatua**

Chapa, kata na towa seti za kadi kutoka **Kielelezo nambari 6.22.** Kadi zipangwe ili kumuonesha mkufunzi majibu sahihi wakati wa kuangalia kazi za kikundi.




Washiriki wakipanga kauli za kutafautisha na kuweka kiunzi nchini uganda

**[Maelezo ya picha: Mshiriki ameshikilia mikononi mwake kipande kidogo cha karatasi chenye taarifa. Mshiriki mwengine anabandika kipande cha karatasi kwenye Chatimgeuzo. Mikono yao tu ndio inayoonekana. Kwenye Chatimgeuzo limechorwa jadweli lenye safuwima mbili. Zenye mada 'kutafautisha' na 'Kusaidia hatua kwa hatua'.]**

Vikundi lazima visome kila kadi na kuamua kama aina ya msaada uliotolewa ni mfano wa mkakati kwa **utafautishaji** au **kusaidia hatua kwa hatua**. Wanatengeneza mirundo miwili ya kadi.

## Kitendo cha 6.5b: Kujumuisha utafautishaji katika upangaji wetu

Kikuu

Muda: Dakika 35

**Maelekezo**
Kitendo hiki kitawasaidia washiriki kufahamu jinsi watakavyoweza kurekebisha vitendo ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye uwezo tafauti.

Kitendo kipo katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza, kwa takriban dakika 10, washiriki watasoma na kujadili baadhi ya miongozo kuhusu njia za utafautishaji kwa wanafunzi wenye uwezo tafauti. Kipindi hiki kitawasaidia kukamilisha sehemu inayofuata ya kitendo ambacho ni kupanga njia ya kutafautisha kazi maalumu za kujifunza.

**Kielelezo nambari 6.23** **Utafautishaji wa kujumuisha uwezo tafauti**

Mpe kila mshiriki **Kielelezo nambari 6.23** na eleza kwamba njia moja wapo ya kupanga vyema kwa utafautishaji wa darasa la wanafunzi wenye uwezo tafauti ni kupanga viwango vitatu kwa kila kazi katika andalio la somo. Mtake mshiriki mmojammoja asome habari kisha wajadili kwa jozi. Ni lazima wabainishe maeneo ambayo yanaweza kuelezewa zaidi na waamue kama ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia walimu.

Kisha watake washiriki kufanya kazi katika vikundi (ikiwezekana, vikundi vilevile vilivyofanya kazi pamoja katika **Kitendo cha 6.3b**).

**Hakikisha kwamba vitendo vya somo vilivyovumbuliwa na washiriki katika kazi 6.3b bado vinaonekana na kisha toa nakala moja ya Kielelezo nambari 6.24 kwa kila kikundi.**

**Kielelezo nambari 6.24** **Mpango wa utafautishaji**

Toa maelekezo yafuatayo:

- Kumbuka mada ya somo/kadi za lengo la kujifunza kutoka **Kielelezo nambari 6.13 (Kitendo cha 6.3b).** Chagua kitendo kimoja ulichoanzisha. (Kumbuka, vitendo vinapaswa kuoneshwa kwenye chumba cha mafunzo).
- Kila kikundi kikamilishe **Kielelezo nambari 6.24,** kinachoonesha jinsi kitendo kilichochaguliwa kinaweza kurekebishwa ili kujifunza kuwe kunaimarishwa kwa wanafunzi ambao hawawezi au wanaweza sana.



Mshiriki akielezea utafautishaji wa kazi ya hisabati ya kikundi chake Zanzibar

**[Maelezo ya picha: Mshiriki mmoja mwanamme amesimama karibu na ukuta akielezea utafautishaji wa kazi ya hisabati ya kikundi chake, huku washiriki wenzie wanaume na wanawake wakimsikiliza.]**

**Mazingatio kwa wakufunzi:** Huu hapa ni mfano unaoweza kutoa ili kuwasaidia washiriki**.**

**Mada ya somo/lengo la kujifunza:** Hisabati-kupanga nambari za desimali kwa mpangilio wa kuanzia ndogo kwenda kubwa na kuanzia kubwa kwenda ndogo.

**Mkakati wa ujifunzaji kwa vitendo kutoka Kielelezo nambari 6.3.** Mchezo wa maswali-wanafunzi wanapaswa kujibu kadi bodi za mwalimu zinazoonesha nambari mbili za desimali kwa wakati mmoja, na kuamua ni ipi ya juu na ipi ya chini. Marekebisho kwa wanafunzi wenye uwezo mdogo: Hakikisha kila mwanafunzi anashiriki, kwa mfano, kwa kumpa kila mwanafunzi nambari ya desimali kwenye kadi na wanapaswa kusimama kwenye mstari unaoonesha 'kushuka' au 'kupanda' (Kadi zinaweza kuwa katika viwango tafauti vya ugumu).

**Marekebisho kwa wanafunzi wenye uwezo zaidi:** Katika kikundi cha wanafunzi wenye uwezo zaidi kufundisha mada au kuandaa chemshabongo kwa ajili ya darasa jengine; au toa seti za kadi za nambari za desimali kwa kila mwanafunzi kupanga kwa mpangilio wa 'kushuka' au 'kupanga' katika viwango tafauti vya ugumu.

Kusanya mrejesho kutoka katika kila kikundi ili wachangiane mawazo na kuyajadili. Wanajadili kama mapendekezo ya marekebisho yanafaa kwa madarasa yao. Mapendekezo yanaweza kuoneshwa kwenye Chatimgeuzo ukutani na kutazamwa na washiriki wakati wa mapumziko.

Kufanya muhutasari wa jinsi ya kujumuisha wanafunzi wenye viwango vya uwezo tafauti kunamaanisha kuwa kila mmoja anashiriki na kujifunza maarifa na ujuzi mpya. Hii inajumuisha wanafunzi wenye uwezo wa juu ambao wanahisi watapata changamoto ya kutoshirikishwa. Wanafunzi wenye uwezo wa chini wanahitaji msaada wa ziada ili wasirudi nyuma na kuvunjika moyo.

# Kitendo cha 6.5c: Utafautishaji wa wanafunzi wenye ulemavu

Kikuu

Muda:  Dakika 60

**Maelekezo**
Kitendo hiki kitasaidia kukuza ufahamu na kujiamini kwa washiriki kwa kurekebisha vitendo vya somo ili kujumuisha **wanafunzi wenye ulemavu kama vile matatizo ya kuona, usikivu au ulemavu wa kutembea.**

Kitendo hiki kipo katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza, kwa takriban dakika 10 washiriki watatazama/kusoma jinsi walimu wanavyobadilisha vitendo vya kujifunza ili viweze kufikiwa na wanafunzi wenye mahitaji ya ziada. Hii itasaidia kukamilisha sehemu inayofuata ya kitendo, ambayo ni kufikiria njia za kurekebisha vitendo vyao vya kujifunza vilivyopangwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wanaopata matatizo ya kuona, kutembea, kukumbuka, kuwasiliana.

Kumbuka kwamba ushauri na muongozo katika Moduli ya ziada ya **kujumuisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada** itakua nyenzo muhimu ya kumbukumbu kwa vitendo hivi.

**Kielelezo nambari 6.25** — **Programu ya video ya EENET 4 – Kutayarisha masomo**

**Kielelezo nambari 6.26** — **Nakala za video**

Washiriki watatazama programu ya video ya EENET's 4- Kutayarisha masomo **(Kielelezo nambari 6.25).** Usisahau kukamilisha mada ndogo. Ikiwa huwezi kufikia video mtandaoni, basi washiriki wanaweza kupewa nakala ya nyenzo ya nakala ya **video (Kielelezo nambari 6.26)** ili waisome kwa jozi. Washiriki pia watahitaji nakala zao za video ya **Kielelezo nambari 6.24** ambazo walizikamilisha wakati wa **Kitendo cha 6.5b.**

Wakiwa katika jozi, washiriki watajadiliana na kuandiaka ujumbe mkuu kutoka kwenye video na kubainisha mbinu muhimu zinazojumuisha upangaji wa somo.

**Mazingatio kwa mkufunzi:** Hii hapa ni orodha kamili ya mbinu zinazoonekana katika video:

- Badili shughuli hizi kwa wanafunzi maalum katika darasa lako, kwa mfano wanafunzi ambao hawawezi kuona, kusikia, au kutembea vizuri.
- Unda baadhi ya vitendo rahisi, au gawanya kazi katika hatua ndogo, kwa wanafunzi ambao wanaugumu wa kufahamu au kukumbuka.
- Kabla ya somo kuanza panga vitabu vyovyote, nyenzo za kuandikia, na vitu vyengine utakavyotumia.
- Unaweza kutengeneza visaidizi vya kufundishia au kujifunzia wewe mwenyewe. Visaidizi vya kufundishia na kujifunzia vinaweza kuwa vitu vilivyokusanywa au kutengenezwa bila malipo, kwa kutumia vitu ambavyo kikawaida hutupwa, kama vile masanduku ya kadibodi, au vifuniko vya chupa.
- Iwapo kuna wanafunzi wenye mahitaji ya ziada darasani hakikisha umetengeneza nyenzo ambazo wanaweza kuzitumia na kuziendesha kwa ajili ya masomo.
- Washirikishe wanafunzi katika kutengeneza nyenzo, kwa mfano, wanafunzi wakubwa wanaweza kusaidia kutengeneza nyenzo kwa ajili ya wanafunzi wa madarasa ya chini. Au wanafunzi wenye uwezo wa kuona wanaweza kusaidia kutengeneza nyenzo za kugusa kwa marafiki zao ambao hawaoni vizuri.
- Boresha upangaji wako wa somo, na utengeneze visaidizi vya ubunifu zaidi vya kufundishia na kujifunzia, kwa kufanyakazi na walimu wengine.

Kisha, watake washiriki waingie katika vikundi vilivyotumika kwenye **Kitendo cha 6.5b** (Kikundi chao cha nyumbani)

Maeneo/Meza tatu zinapaswa kutengwa kwenye chumba kwa ajili ya ‘vikundi 3 vya wataalamu’. Wazo ni kwamba kila kikundi kitume mjumbe au wajumbe kwenye meza hizi kujadili jinsi ya kurekebisha zaidi vitendo vyao vya somo ili kujumuisha wanafunzi wenye **ulemavu wa uoni, ulemavu wa usikivu na ulemavu wa kutembea.**

Kitake kila kikundi (ambacho tunaweza kukiita kikundi cha nyumbani) kujigawa wenyewe na vitawanyike ili wakae kwenye meza tatu za ‘vikundi vya wataalamu’. Kwahivyo, kila kikundi kati ya ‘vikundi hivi vya wataalamu’ kitakuwa na mshiriki mmoja kutoka kwenye kila kikundi cha nyumbani.

**Kielelezo nambari 6.27** **Msaada kwa wanafunzi wenye ulemavu**

Toa kadi moja kwa kila kikundi cha wataalamu kutoka kwenye kadi tatu zilizokatwa kwenye **Kielelezo nambari 6.27**. Kuna 'angalia' kadi, kadi ya 'usikivu', na kadi ya 'kutembea'.

Kila 'kikundi cha wataalamu' kiangalie kadi yao. Kadi inapendekeza mawazo ya njia za kurekebisha na kuendeleza vitendo ili kuwajumuisha wanafunzi wenye mahitaji hayo. Watajadili mawazo haya na kupendekeza mifano zaidi, ikijumiisha njia za kurekebisha vitendo ambavyo tayari waliviunda wakati wa Moduli hii.

Baada ya takriban dakika 10-15 watake washiriki wajiunge tena na kikundi chao cha nyumbani.

**Kielelezo nambari 6.28** **Kurekebisha vitendo vya wanafunzi wenye ulemavu**

Sasa kipe kila kikundi nakala ya **Kielelezo nambari 6.28** chenye maelekezo yafuatayo:

- Angalia Kielelezo nambari 6.28.
- Angalia tena nakala zako zilizokamili za Kielelezo nambari 6.24. (Hizi zinaweza kuoneshwa). Hizi zinaonesha jinsi utakavyotafautisha vitendo vya wanafunzi wenye uwezo mdogo au mkubwa ili kusaidia lengo la ujifunzaji zilizochukuliwa kutoka Kielelezo nambari 6.13.
- Katka vikundi vyenu, tumia taarifa mlizokusanya wakati mlipokuwa mnazitembelea 'meza tatu za wataalamu' ili kukusaidia kukamilisha Kielelezo nambari 6.28. Onesha jinsi unavyoweza kurekebisha kitendo chako ili wanafunzi wenye shida ya kuona, kusikia, kutembea, kufahamu, kukumbuka, kuwasiliana zinajumuishwa.

**Mazingatio kwa mkufunzi:** huu hapa ni mfano unaoweza kutoa ili kuwasaidia washiriki.

**Mada ya somo/lengo la kujifunza:** Hisabati-kupanga nambari za desimali kwa mpangilio wa kupanda na kushuka.

**Kitendo:** mchezo wa maswali- ambapo wanafunzi wanapaswa kujibu kadi za mwalimu zinazoonesha nambari za desimali kwa wakati mmoja, na uamue ni ipi ya juu au ya chini.

**Kurekebisha wanafunzi ambao wanashida ya kuona:** Tumia kadi kubwa sana, vipande vikubwa vya karatasi, kadi zilizoandikwa nambari kubwa za desimali. Rangi bora ya kutumia kwa wanafunzi wenye uoni hafifu ni picha nyeusi kwenye mandhari nyuma nyeupe au njano. Wakati wa chemshabongo hizi zinaweza kuoneshwa mbili kwa wakati mmoja wanafunzi wanaulizwa kuziweka katika mpangilio wa kupanda/kushuka. Vyenginevyo, wakati wa chemshabongo idadi kubwa sana huwekwa kwenye meza mbele ya mwanafunzi mwenye uoni hafifu ili wasiangalie umbali mrefu kuona kadi ukutani au kushikiliwa na mwalimu.
Kurekebisha wanafunzi wenye uzito wa kusikia: wakati suali la chemsha bongo linapoulizwa na kuoneshwa (tazama urekebishaji wa wanafunzi wanaoona hapo juu), hakikisha suali linasomwa na kuoneshwa ubaoni/ukutani au kwenye karatasi ya kitini. Ni muhimu kujumuisha mchoro/picha na kila suali la chemsha bongo (ikiwa inafaa na haitoi jibu).

Kurekebisha kwa wanafunzi ambao wana shida ya kutembea: tengeneza na tumia kishikilia hati kwa kadi – fremu ya kuzionesha – ikiwa mwalimu atatoa kadi kwa vikundi ili kupanga katika mpangilio wa kupanda/kushuka. Fremu hii inahakikisha kwamba kadi zinaweza kusogezwa karibu na mwanafunzi.




Mtaalamu anarudi katika kikundi chake ili kuwashauri kuhusu kurekebisha kitendo chao kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu Zanzibar

**[Maelezo ya picha: wanawake wawili na wanaume watatu wamekaa katika meza moja. Mwanamke mmoja anatoa maelezo na wengine wanamsikilizo]**

Ikiwa kikundi kinafikiri kitendo chao tayari kinaweza kufikiwa na wanafunzi wanaopata matatizo haya, wanapaswa kueleza kwa nini. Kisha, kama maelezo yanaonekana kuridhisha, wanaweza kuangalia **Kielelezo nambari 6.13** tena na kuunda mkakati tendaji kwa kujifunza kwa kufundisha lengo tafauti la kujifunza kutoka **Kielelezo nambari 6.13,** kwa pamoja wakipendekeza jinsi inavyoweza kubadilishwa kwa wanafunzi wenye matatizo ya uoni, usikivu, au kutembea.

Orodhesha kwa ufupi mawazo kutoka kwa kila kikundi ubaoni au Chatimgeuzo. Unaweza kuwa na vichwa vya habari 3 kwenye safu wima- kuona, kusikia na kutembea.

Hatimaye, washiriki wanaweza kuangalia vikundi vya masomo ya utafautishaji yaliyokamilika wakati wa matembezi ukumbini, ambapo wanakikundi wanaeleza mawazo yao na kuchukuwa maswali kutoka kwa wenzao.



Utafautishaji wa kikundi cha shughuli zao za sayansi kwa wanafunzi wenye ulemavu

**Virekebisha vitendo kwa wanafunzi wenye ulemavu**

| | |
|---|---|
| Somo/lengo la kujifunza<br>Kitendo | - Sayansi/mimea<br>- Kufanya majaribio ili kujua masharti muhimu kwa ajili ya kuota kwa mbegu |
| Je! Utarekebisha vitendo kwa wanafunzi ambao wanashida ya kuona? | Matarajio ya uotaji wa mbegu<br>Makundi mchanganyiko, utatuzi wa matatizo shirikishi<br>- Rekodi ya sauti<br>- Rafiki msaidizi<br>- Mpangilio wa ukaaji<br>- Vitendo vya kugusa.<br>- Matumizi ya rangi tafauti.<br>- Kutayarisha nyenzo za nukta nundu. |
| Utarekebisha vipi kitendo kwa wanafunzi ambao wanaulemavu wa usikivu vizuri? | - Rafiki msaidizi<br>- Tafauti za IMS<br>- Vikundi mchanganyiko.<br>- Uwasilishaji<br>- Lugha chanya.<br>- Maoni kwa wakati. |
| Utarekebisha vipi kitendo kwa wanafunzi ambao hawawezi kutembea kwa urahisi? | - Rafiki msaidizi<br>- Kuwajibika kwa mwenyekiti/kuwasilisha/kuchukua dokezo<br>- Kupata aina mbali mbali za IMS |



Washiriki wanajadili mpango wa utafautishaji

**[Maelezo ya picha: karatasi nne za Chatimgeuzo zinaning'inia ukutani nje ya jengo. Karatasi hizo zina majadweli yenye maandishi. Wanawake watano na wanaume wanne wanaziangalia na mwanamke mmoja anaashiria kwenye chatimgeumzo kwa fimbo.]**



Matembezi ya ukumbini

**[Maelezo ya picha: Katika picha zote mbili, wanawake na wanaume wamesimama mbele ya karatasi ya Chatimgeuzo ukutani. Kwenye picha ya upande wa kushoto wako sehemu ya nje na migongo yao imeelekea kamera. Picha ya upande wa kulia wamo ndani, na nyuso zao tunaziona zinatabasamu.]**

# Kipindi cha 6.6: Kutumia tathmini ili kusaidia ujifunzaji

## Utangulizi

Kutumia upimaji katika kusaidia ujifunzaji, ni mkakati muhimu sana wa ujifunzaji mahiri kwa ujumuishaji. Hii ina maana walimu wanaweza kupanga kwa umahiri kila kinachohitajika kujifunza, kuwasilisha kwa wanafunzi na kubuni na kurekebisha kazi ili kuhakikisha kila mwanafunzi anaweza kupata mafunzo. Kipindi hiki kinazingatia njia za kutumia upimaji ili kusaidia ujifunzaji, ikijumuisha kutoa mrejesho mzuri na kuuliza maswali bora. Maswali mawili muhimu ambayo walimu wanapaswa kuzingatia kila wakati ni:

- Je! ninataka mwanafunzi afanye nini?
- Je! ninataka mwanafunzi ajifunze nini?

Washiriki kukumbushwa kazi waliyofanya katika **Moduli ya 4** 'kuchunguza na kutambua mahitaji ya kujifunza'.

Inapaswa kusisitiza kuwa upimaji rika na upimaji binafsi ni dhana yenye nguvu sana kufundishia na ni muhimu katika upimaji wa mchakato wa kujifunza. Hili litachunguzwa zaidi katika Moduli ya baadae inayolenga ushiriki wa wanafunzi katika kujifunza wenyewe.

## Kitendo cha 6.6a: Kutumia upimaji kwa kujifunza

Kikuu

Muda: Dakika 35

**Maelekezo**
Kitendo hiki kitaendeleza zaidi matumizi ya taarifa za upimaji wa washiriki ili kuendeleza ujifunzaji.

Kabla ya kuweka kazi, eleza istilahi zifuatazo za upimaji:

- 'Upimaji' wa ujifunzaji, au 'upimaji wa mwisho, humjulisha mwalimu kama mwanafunzi ametimiza malengo ya kujifunza. Upimaji huu kwa kawaida hufanyika mwishoni mwa somo au kitengo cha kazi.
- 'Upimaji wa ujifunzaji' au 'upimaji endelevu', husaidia kutambua ni kwanini mwanafunzi hufanya kama anavyofanya na jinsi mwanafunzi anavyoweza

kuimarisha. Mifano ya upimaji endelevu ni pamoja na kuchunguza na/au kuhoji wanafunzi wanapofanya kazi. Hii ina maana kwamba mwalimu anaweza kurekebisha ufundishaji wa somo katikati au kurekebisha andalio lao la somo linalofuata ili kuhakikisha malengo ya kujifunza yanafikiwa.

Washiriki watafanya kazi katika vikundi na watatambulishwa kupitia hali ifuatayo:
Baada ya darasa zima kuangalia baadhi ya hadithi na vitabu vya wanafunzi chipukizi, na kujadili jinsi vinavyoundwa, mwalimu atawapa wanafunzi kazi ifuatayo:

**Andika hadithi ambayo unaweza kusoma kwa wanafunzi chipukizi.**
Mwalimu atazunguka darasani na kuangalia kazi za wanafunzi wakati wanafanya hivyo. Mwalimu ataangalia ikiwa kila mmoja anafanya kazi.

Eleza kwamba ni vigumu sana kumuangalia kila mwanafunzi, hasa katika madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Kwa hivyo, washiriki wanapaswa kutambua kwamba mwalimu katika hali hii atatumia maarifa yake juu ya kutambua ni wanafunzi wepi wanaohitaji uangalizi zaidi au hawakuwa na uangalizi kwa muda fulani.

Unaweza kutumia mfano ufuatao: Mwalimu katika kisa anafahamu mwanafunzi anayeitwa Patima ambaye anashida ya uandishi: ujuzi wake wa kusoma na kuandika haujakuzwa. Walakin, anafurahia kuchora.

Waulize washiriki jinsi mwalimu anavyoweza kuingilia kati ili kumsaidia Patima katika kazi ya uandishi wa hadithi. Sisitiza kwamba kuingilia kati kwa mwalimu kunaweza kuchukua muda wa sekunde au dakika moja tu, kwa vile ana wanafunzi wengine darasani wa kuwahudumia. Kwa ajili ya kumbukumbu ya mkufunzi majibu ya washiriki yanaweza kujumuisha:

- Mwalimu anapendekeza Patima achore hadithi yake kwa kutumia maelezo rahisi sana.
- Mwalimu ametayarisha vifaa vya kumsaidia Patima na vyengine kwa wanafunzi wenye matatizo sawa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kumpa Patima kielelezo chenye maswali rahisi ili kumsaidia kupanga mawazo kama vile: ‘Nani muhusika wako mkuu?’ ‘Anafanya nini?’ au mwalimu anaweza kumpa Patima orodha ya maneno/msamiati ambao amejifunza hivi karibuni na kuona kama anaweza kuutumia kutunga hadithi fupi.

**Kielelezo nambari 6.29** **Hatua za kusaidia ujifunza**

Toa **Kielelezo nambari 6.29** kwa kila kikundi na ueleze kuwa zoezi lifuatalo linazingatia njia ambazo mwalimu anaweza kuimarisha ujifunzaji kupitia muingiliano wao na kila mwanfunzi. Sasa wape washiriki maagizo yafuatayo:

- Soma kwa sauti kila mmoja anachosema kuhusu jinsi wanafunzi 5 wanavyoendelea na kazi.
- Andika katika safu wima ya pili njia unazofikiri angeweza kujibu kila mwanafunzi.
- Kila kikundi kijadili mwanafunzi mmoja baada ya mwengine.

Baada ya kama dakika 15, mpitie kila mwanafunzi na vitake vikundi kuwasilisha baadhi ya mapendekezo yao. Haya yanapaswa kujadiliwa.

**Mazingatio kwa mkufunzi**

Baadhi ya mawazo:

**Halima:** Onesha baadhi ya sentensi za mwanzo za hadithi kwa wanafunzi wadogo (kwa mfano, ‘Hapo zamani za kale kulikuwa na…)

**Hamad***:* Mtake Hamadi asome sehemu ya hadithi yake kwa sauti na umuoneshe yalipo mapumziko ya asili. Kisha mtake aweke vituo mahali pa mapumziko hayo, kabla ya kuendelea kuandika (Kwa uakifishaji).

**Mwana***:* Pendekeza Mwana aandike hadithi kuhusu msichana aliyepoteza bangili yake na kuitafuta kijijini, akiwauliza watu katika kila nyumba ikiwa wameiona.

**Abdullah:** Angalia kama kuna marekebisho yoyote ambayo anaweza kuyafanyia kazi na kumpa shughuli ndefu kama vile kuunda jalada la kitabu kwa ajili ya hadithi yake, kuelezea sehemu za hadithi kwa michoro au kuandika barua kwa darasa la vijana au skuli ya Maandalizi/msingi, kuuliza kama yeye na darasa lake wanaweza kutembelea ili kuwasomea hadithi.

**Fatma***:* Tabasamu na onesha kwamba umeona juhudi zake.

Mwisho, watake washiriki kufikiria kuhusu taarifa ambayo mwalimu alipata kutokana na kuzunguuka darasani walipokuwa wakifanyakazi ya kuandika hadithi. Vipi maarifa haya yanaelezea mpango wa mwalimu wa kazi ile ile kwa mara nyengine- mfano, vipi mwalimu anatumia taarifa hizi kufanya mabadiliko na maboresho?

Kwa sababu ni vigumu kumchunguza kila mwanafunzi katika darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi wakati wa somo, ni muhimu kuhakikisha kwamba upimaji wa kujifunza uelekeze mabadiliko ya upangaji wa somo, na kuwa inajumuisha **uchunguzi wa wanafunzi katika uwezo mpana**.

## Kitendo cha 6.6b: Maoni ili kuimarisha ujifunzaji

Kikuu

Muda: Dakika 40

**Maelekezo**

Kitendo hiki kitakuza matumizi bora ya maoni yanayotolewa kwa wanafunzi.

Eleza kwamba wanafunzi hufanya vyema zaidi wanapochukua jukumu la kujifunza wenyewe, kujua maendeleo yao na kile wanachohitaji kujifunza baadae. Ili kufanya hivyo wanahitaji maoni sahihi, yaliyowasilishwa kwa uwazi na yenye kujenga. Wanahitaji kujua malengo yao ya kujifunza, kile wanachofanya vizuri, mapungufu katika kujifunza kwao ni nini, na jinsi wanavyoweza kuimarisha. Hii inamaanisha kuwapa wanafunzi muongozo, sio alama tu.

Kitendo hiki kipo katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza, kwa takriban dakika 10, washiriki wasome kuhusu kutoa maoni. Hii inasaidia washiriki kukamilisha sehemu ya pili ya kitendo, ambayo inahusisha hali ya igizodhima la darasani ili kufahamu vyema athari za maoni, na kuyafanya yawe ya kujenga zaidi.

**Kielelezo nambari 6.30** — **Maoni muhimu**

**Kielelezo nambari 6.31** — **Fanya na usifanye**

Watake washiriki kufanya kazi katika jozi na wape kila jozi nakala ya **Kielelezo nambari 6.30** na **Kielelezo nambari 6.31**. Kisha watake wasome vielelezo vyote

viwili. Baada ya kusoma kielelezo **nambari 6.30,** wanahitaji kuwamua ni maelezo yepi ya maoni katika **Kielelezo nambari 6.31** yanafaa na yepi hayafai. Wanaweza kuandika maandishi kwenye karatasi au kando kwenye kipande cha karatasi tupu yenye vichwa viwili vya safu wima- 'inafaa' (au 'fanya') na **'haifai'** (au 'usifanye').

Hatimaye, watake washiriki kubadilishana mawazo kwa kile walichokiamua kisha waelezee na kujadili maamuzi yao.



Kujadili mambo ya kufanya na kutokufanya Zanzibar

**[Melezo ya picha: Wanaume wawili na wanawake watano wamekaa katika viti huku wakiwaangalia wanawake wawili waliokaa sakafuni wakiandika kazi ya kujadili mambo ya kufanya na kutokufanya Zanzibar]**

**Mazingatio kwa mkufunzi:** Yafuatayo yanaweza kuwa majibu yenye **ufanisi.**

- "Hilo ni wazo zuri, na linaweza kufanya kazi vizuri zaidi ikiwa....".
- "Nimeweka alama mahala ambapo wamekosa vituo kamili au kituo kidogo. Unaweza kujaribu kuweka alama ya uwakifishi sahihi?"
- "...Mwishowe, ulitakiwa kufanya muhutasari wa matokeo yako lakini hukufanya. Asha anaweza kuonesha yake kama mfano na jinsi unavyoweza kufanya hivi...".
- "... Ndio bado kuna kazi nyingi za kufanya lakini nilifurahishwa sana na juhudi zako."
- "Wiki iliyopita umehangaika na hili lakini sasa ...".

Yafuatayo yanauwezekano wa kuwa ni majibu **yasiyofaa**.

- "Sijui. Inaonekana kwangu kuwa halina maana…".
- "Wanadarasa wengine wanafahamu kwa nini huelewi?"
- "Sijali Kama huna Mstari, Wakati mwengine nataka vipimo sahihi".
- "Endelea, toa maarifa maarifa yako ya hapo awali na uniambie umemaanisha nini".
- "Soma hili darasani ili waone jinsi ulivyo mvivu".

Ni muhimu, hasa katika mazingira ambapo Kiengereza ni lugha ya ziada kwamba mkufunzi kuruhusu tafsiri za jibu 'lenye ufanisi' au 'isiofaa' kubadilika, ingawa maneno haya yanahitaji kuelezewa masharti ya utendaji mzuri wa ujumuishaji.

Wakumbushe washiriki maswali mawili muhimu ambayo walimu wanapaswa kukumbuka kila wakati.

- Je! Ninataka mwanafunzi afanye nini?
- Je! Ninataka mwanafunzi ajifunze nini?

**Kielelezo nambari 6.32** **Kadi za maoni za Igizodhima**

Watake washiriki wakae katika vikundi vya watu wanne ikiwezekana, wakichagua watu ambao hawajawahi kukaa nao hapo awali. Ikiwa kuna zaidi ya vikundi vinne vya washiriki wa ziada wanapaswa kupewa jukumu la kuwa 'watazamaji'

Wapatie kila kikundi seti ya kadi ya **Kielelezo nambari 6.32**, kadi moja kwa kila kikundi pamoja na penseli 2 na vipande 2 vya karatasi ya kuchora kwa kila kikundi. Kadi ikabidhiwe kwa washiriki wakiwa wameinamia chini.

Mtake kila mshiriki achukuwe kadi yake, aisome bila ya kuionesha kwa kikundi, na aitunze bila ya kuifunua kwa wengine. Washiriki wawili katika kila kikundi ni 'wanafunzi' na wawili ni 'walimu'. Mtake kila mshiriki achukue dakika chache kujiandaa kuwa katika jukumu.

Kila mtu anapokuwa tayari, tangaza kazi ambayo ‘wanafunzi’ ni lazima waanze moja kwa moja. Kwa kutumia penseli na karatasi iliyotolewa, waambie ‘wachore nyumba na kiwanja cha bustani kwa dakika 3.

Tangaza kuwa kazi imeanza na, baada ya dakika 3, tangaza kwamba ‘wanafunzi’ lazima wasitishe. Wakati wa dakika 3 hakikisha kwamba ‘walimu’ katika kila kikundi wanasimama na kuangalia kwa karibu kila ‘mwanafunzi’ katika kikundi chao kwa zamu wakitoa mrejesho wanapotazama kila ‘mwanafunzi’ wakichora.

Washiriki waliobakia wamepewa majukumu ya kuwa ‘watazamaji’, na lazima waangalie muingiliano kwa makini na wawe tayari kutoa maoni mwishoni mwa kitendo.

Mara baada ya ‘wanafunzi’ kuwacha kuchora, ‘walimu’ wanaweza kuwa na dakika nyengine ya kumaliza kutoa maoni yao kwa kila ‘mwanafunzi’. Vitake vikundi vitoke nje ya majukumu yao na kufanya yafuatayo

- ‘Wanafunzi’ katika kila kikundi washiriki wanabadilishana uzoefu kwenye vikundi vyao athari za mrejesho waliopokea kutoka kwa ‘walimu’ wawili- jinsi ulivowafanya wajisikie na kile walichojifunza.
- ‘Walimu’ Katika kila kikundi wanabadilishana uzoefu wao wa kutoa maoni.
- ‘Watazamaji’ wote hubadilishana mawazo kwa kile walichokiona wakati wa igizo dhima.

Kisha walete washiriki wote pamoja ili kubadilishana mawazo katika baadhi ya mambo muhimu yaliotolewa katika kila kikundi. Sisitiza yafuatayo:

- Maoni ni kutoa taarifa kwa mtu binafsi ambayo inaangalia utendaji au tabia zake.
- Maoni yanayotolewa yanapaswa kutolewa kwa njia chanya na kupelekea hatua ya kuthibitisha au kuendeleza utendaji au tabia ya mtu binafsi.
- Maoni yanayotolewa hayafai kuwa ya mtu binafsi na yanapaswa kuzingatia data, ukweli au mifano iliyozingatiwa ya ushahidi.
- Maoni yasiwe ya kuwakosoa wanafunzi kwa kutofanya jambo ambalo halikuwa hitaji lililoainishwa katika maigizo. Hii itakuwa si haki na inaweza kukuza kutoaminiana.

Hatimaye, kikundi kizima kijadili maswala yoyote zaidi yanayotokana na kutoa maoni yenye kujenga darasani.

# Kitendo cha 6.6c: Kuuliza maswali bora

Kikuu

Muda: Dakika 20

**Maelekezo**

Kitendo hiki kitaongeza ufahamu wa umuhimu wa kuuliza maswali ambayo yanaimarisha ujifunzaji, kuhusisha wanafunzi katika somo kwa kufikiri na kumpa mwalimu ufahamu wa kiwango cha ujifunzaji.

Washiriki kufanya kazi kwa jozi.

**Kielelezo nambari 6.33** **Maswali Bora**

Wapatie kila jozi nakala ya **Kielelezo nambari 6.33** na waambie waisome. Kisha kitake kila kikundi kutumia dakika chache kufikiria swali la mfano au mwanzo wa swali ili kuelezea hadi nukta tatu. Kwa mfano:

- Nambari 2 ('Imarisha mafunzo ya awali'), washiriki wanaweza kupendekeza swali kuanzia:
  'Eleza kwa nini …?' 'Sema nini …?' 'Lini…?'

- Nambari 6 ('Kuongeza fikra kutoka halisi hadi uchambuzi'), Washiriki wanaweza kupendekeza swali kama:
  'Niambie muhusika alifanya nini mwishoni mwa hadithi na kupendekeza kwa nini?'

- Nambari 9 ('Himiza fikra bunifu na utatuzi wa matatizo'), washiriki wanaweza kupendekeza swali kuanzia;
  'Fanya kwa nini…?'

**Kielelezo nambari 6.34** **Baadhi ya mikakati ya kuuliza maswali**

Mwisho, wape washiriki **Kielelezo nambari 6.34** ili wasome na kuhifadhi kwa marejeleo ya siku zijazo kama mfano wa baadhi ya mikakati ya kuuliza maswali. Wewe na washiriki mnaweza kujadili nyenzo hii ili kuelewa kila mkakati.

# Kipindi cha 6.7: Kutumia utafiti tatuzi ili kukuza ujifunzaji mahiri

## Utangulizi

Tukikumbuka utafiti tatuzi uliofanywa awali, ni muhimu kusisitiza tena jinsi kila skuli ilivyo na changamoto na fursa za kipekee katika elimu, zinazohitaji majibu ya kipekee. Kwahivyo, walimu hawawezi kutegemea 'wataalamu' kutoka mahali pengine kuwaelekeza jinsi ya kuifanya skuli yao iwe jumuishi.

Walimu-pamoja na wanafunzi, wazazi/walezi na wanajumuiya wengine wa skuli wanahitaji kuwa wataalamu kwenye mazingira yao wenyewe. Wanahitaji kuwa na uwezo wa kuchunguza kile kinachotokea katika skuli na jumuiya zao, na kutambua vikwazo vya mjumuisho vinavyohitaji kushughulikiwa, au suluhu za ujumuishi zinazohitaji kuongezwa.  Kisha (Kwa msaada wa wengine) kuanza kuchukua hatua zinazohusika. Utafiti tatuzi ni muhimu sana kwa hili. Inasaidia wadau kuangalia hali zao, kuchanganua matatizo, kupendekeza ufumbuzi na kisha kuchukua hatua.

## Kitendo cha 6.7: Kuamua lengo

Kikuu

Muda: Dakika 40

**Maelekezo**

Kitendo hiki kitawapa washiriki fursa ya kuamua lengo lao la utafiti litakuwa nini.

Wape washiriki maagizo yafuatayo:

- Kila mmoja afikirie kazi aliyoifanya kwenye moduli hii kisha aandike lengo la kila kipindi.
- Ukifikiria vipindi vyote, amua ungependa utafiti tatuzi wako ulenge kitu gani. Fikiria kwa nini, na ufikirie ikiwa ni lengo ambalo utaweza kuzingatia. Unaweza kutaka kukumbuka/kupitia upya 'maono' na 'malengo' uliyoamua katika **Kitendo cha 6.1c** na mabadiliko uliyorikodi kwenye **Kielelezo nambari 6.4** ambayo ulisema yangehitajika ili malengo yako yatimie. Hii inaweza kukusaidia kuamua unachotaka kuchunguza zaidi.

- Katika utafiti tatuzi wako unaweza pia kufikiria njia za kuwashirikisha wanafunzi, ikiwa ni pamoja na wale ambao wana mahitaji ya ziada, katika kujibu matokeo.
- Jadili maamuzi yako na vikundi/timu nyengine na uhakikishe kuwa yanawezekana. Jaribu na ufikirie njia bunifu za kuwashirikisha wanafunzi katika kufanya utafiti.

Washiriki watoe mrejesho kuhusu baadhi ya mada walizochagua za utafiti. Kikundi kizima kinaweza kujadili kama mada zilizochaguliwa zinaonekana kutekelezeka. Hatimaye watake washiriki kwa pamoja wawasilishe lengo lao la utafiti kwa **njia ya uchunguzi au swali**.

**Mazingatio kwa mkufunzi:** maswali yafuatayo yanaweza kujitokeza kutokana na mada kuu zilizojadiliwa katika moduli hiyo:

- Je! mazingira ya darasani yako tayari kwa kujifunza kwa vitendo? kama ndiyo, kwa nini? Ikiwa hapana, kwa nini?
- Je! mwalimu anatumia mikakati yoyote ya ujifunzaji mahiri? ikiwa ndio, ni ipi hiyo? kama hapana, ni mikakati gani ya kufundishia inayotumiwa sasa?
- Je! kuna kazi ya jozi au ya kikundi? Je! Ina ufanisi kiasi gani? Tunajuaje?
- Je! walimu wanatafautisha wanafunzi wenye uwezo au ulemavu tafauti? Ikiwa sivyo, hiyo inaathiri vipi ujifunzaji? Kama ndio, toa mifano na ushahidi wa jinsi inavyoathiri ujifunzaji.
- Je wanafunzi hupokea mrejesho wa aina gani? Je! Ni chanya au hasi? Je! hii ina athari gani katika kujifunza?
- Kuna suali gani darasani? Je kuna ushahidi wa walimu kutumia mbinu za kuuliza masuali? Je! masuali yanaonekana kuwa na matokeo gani katika kujifunza?

# Vielelezo

Moduli

6

## Kielelezo nambari 6.1 Majibu tendaji na yasiyo tendaji

| Majibu yasiyotendaji | Majibu tendaji |
|---|---|
| …huathiriwa zaidi na: | …iwa zaidi na: |
| • Mazingira yao ya kimwili -mtazamo na hisia zao hubadilika kulingana na hali zinazowazunguka | • Maadili yaliyowekwa kwa uangalifu |
| • Mazingira yao ya kijamii –mitazamo na hisia zao hubadilika kulingana na jinsi wengine wanavyowatendea au hisia za wengine | • Imani kwamba wanaweza kuchagua majibu yao kwa kile kinachotokea kwao |
| • Imani kwamba wao ndivyo walivyo leo kwa sababu ya vinasaba vyao, maisha yao ya zamani na mazingira yao ya sasa, na kwamba kuna kidogo wanachoweza kufanya ili kuleta mabadiliko. | • Imani kwamba wao ndivyo walivyo leo kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya chaguzi walizofanya jana |

## Kielelezo nambari 6.2: Taarifa tendaji na zisizo tendaji

"hakuna ninachoweza kufanya"

"ananitia wazimu sana"

"lazima"

"hebu tuangalie nini tunaweza kufanya"

"hawataruhusu hili"

"ninaweza kubadilika"

"kama tu"

"ndivyo nilivyo"

"nachagua"

"nita"

"ninajitolea"

"lazima"

"napendelea"

"siwezi"

"naweza"

# Kielelezo nambari 6.3: Kadi ‘za dira yetu’

Nakili na ukate seti za kadi hizi kwa kila kikundi kidogo.

| | |
|---|---|
| “mahitaji ya kila mwanafunzi hujulisha upangaji wa somo.” | “Ufundishaji wetu ni rahisi na tunatumia mikakati mingi ya ufundishaji ili kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi wote.” |
| “wanafunzi wote wanahisi utambulisho wao wa kitamaduni unaheshimiwa na kwamba wako salama wanapokuwa skuli.” | “Tunatumia upimaji kuimarisha ujifunzaji badala ya kuwatenga wanafunzi kujifunza, kutambua ushahidi wa kujifunza ili kuwasaidia wanafunzi kuendelea kujifunza.” |
| “wanafunzi wote wanafurahia masomo yao na wanayatumainia.” | “Tunapanga vitendo vya kukuza uhusiano mzuri kati ya wanafunzi.” |
| “Tunamatarajio makubwa kwa wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wale wenye mahitaji ya ziada.” | “Tunabuni mtaala wetu kulingana na mahitaji, uwezo na matarajio ya wanafunzi wetu.” |
| “Masomo yetu yanamlenga mwanafunzi kujifunza kuwa shirikishi: Sisi ni wabunifu katika matumizi yetu ya rasilimali chache.” | “Wanafunzi wetu wanafahamu malengo ya kujifunza ya kila somo na vitendo vyetu vinakuza ujifunzaji wa kujitegemea.” |


## Kielelezo nambari 6.4: Kutambua malengo yetu

| |
|---|
| Lengo langu ni… |
| |

# Kielelezo nambari 6.5: Picha za darasani


(Chanzo: EENET (2017) 'Siku ya Elimu Mjumuisho', muongozo wa mafunzo ya video, mpango wa 5, Kitini 5a)

Picha ya 1



Zambia, EENET

Picha ya  2




Zambia, EENET

Picha ya 3




Cambodia, Nicolas Axelrode / HI

Picha ya 4



Mozambique, E. Schurman

Picha ya 5



Burkina Faso, S. Imerovic

## Kielelezo nambari 6.6: Kujibu picha za darasani

Tazama na jadili picha za madarasa katika **Kielelezo nambari 6.5**. Fikiria na andika vidokezo katika masuali yafutayo:

| Picha | Mambo mazuri | Changamoto | Ni wanafunzi gani wanaweza kutatizika? |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

# Kielelezo nambari 6.7: Mabadiliko yanayopendekezwa

- Angalia tena picha zile zile (kikundi chako kinapaswa kuanza na picha ile ile kama mara ya mwisho).
- Jibu maswali haya:

1. Ni mabadiliko gani rahisi unaweza kufanya katika madarasa haya ili kuhakikisha kuwa:
    - Wanafunzi wajihisi wapo salama na wamestarehe zaidi;
    - Wanafunzi wanaweza kuona au kusikia zaidi;
    - Wanafunzi na walimu wanaweza kuzunguka kwa urahisi zaidi.

2. Ni mabadiliko gani yanahitajika ambayo hukuweza kufanya peke yako ukiwa ni mwalimu?
    - Eleza mabadiliko.
    - Eleza ni nani mwengine anayehitaji kuhusika na kwa nini.

| **Nambari ya picha** | **Mabadiliko gani rahisi unaweza kuyafanya?** | **Ni mabadiliko gani yanahitajika ambayo hukuweza kufanya ukiwa ni mwalimu?** |
|---|---|---|
| | | |

## Kielelezo nambari 6.8: Kuandaa mazingira halisi ya darasa

Nakili na ukate kadi hizi na ukipe kila kikundi seti moja. (Unapaswa kuwa na kadi 5 za 'Kazi kuu za kupanga' na kadi 13 za 'vitendo vya kuunga mkono')

| Kuandaa kazi kuu | Vitendo vya kuunga mkono |
|---|---|
| Ongeza nafasi ya darasani | Ondoa samani zisizohitajika, kupunguza ukubwa wa dawati la mwalimu ikiwa ni lazima. |
| | Fikiria kutumia mikeka, matakia au zulia (badala ya viti/meza) vinavyoweza kuwekwa nje kwa muda na hata kutumika humo kwa masomo fulani. |
| | Hakikisha kila mwanafunzi anaweza kuona ubao mkuu na kuweka mbao ndogo kadhaa za kuandikia kuzunguka chumba kwa ajili ya kazi ya kikundi. |
| Kuwezesha matembezi | Weka taratibu za kuingia na kutoka (kwa mfano, hakikisha kwamba wanafunzi waliokaa nyuma wanaingia mwanzo na kuondoka mwisho). |
| | Panga harakati mapema ili kuhakikisha unapunguza usumbufu (kwa mfano, wakati wa kutembea kutoka kukaa kwa safu kwa ajili ya jaribio, kupanga vikundi kwa ajili ya vitendo vya sayansi). |
| | Panga mapema ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaweza kupata nyenzo wanazohitaji na wale wenye mahitaji ya ziada wanaweza kuvifikia vitendo. |

| | |
|---|---|
| **Tumia nafasi nje ya darasa** | Zunguka eneo lote la skuli yako na utambuwe maeneo mazuri ya nje ya kujifunzia. |
| | Tambua maeneo ambayo wanafunzi wanaweza kufanya kazi kwa usalama, na ambao miradi fulani inaweza kufanyika (kwa mfano, mahali pa igizodhima na utendaji au uchunguzi wa hisabu). |
| | Hakikisha wanafunzi wanafahamu kabla ya kuondoka kwenye chumba, wafuatilie wakiwa nje na hakikisha wote wanakutana pamoja mwishoni ili kujibu kazi yako. |
| **Onesha kazi za wanafunzi** | Kuwa mbunifu na uoneshe kazi kwenye kuta na milango au hata kuning'inia kutoka darini. Onesha kazi kwenye sehemu ya ubao wakati wa somo. |
| | Tumia kamba, Vibanio, ukanda au hata miba butu. |
| **Washirikishe wanafunzi** | Wape wanafunzi majukumu ya kusaidia kudhibiti nafasi ya darasa (kwa mfano, kuunda mbao za maonyesho au maonesho ya ufuatiliaji). |
| | Watake wanafunzi wapendekeze suluhu ya tatizo linapotokea. |
| | Mwanzoni mwa mwaka watake wanafunzi wapendekeze njia za kuimarisha nafasi halisi. |

Majibu kwa mkufunzi:

- Kadi za 'kitendo kinachosaidia' katika safu wima ya kulia zimepangwa kando ya kadi za 'majukumu ya kupanga' wanazotumia.

# Kielelezo nambari 6.9: Kuandaa mazingira darasani kisaikolojia na kijamii

Nakili na ukate kadi hizi na kipe kila kikundi kidogo seti moja. (Unapaswa kuwa na kadi 5 za ‘kadi kuu za kupanga’ na kadi 14 ‘za ‘kusaidia hatua)

| Kazi kuu za kuandaa | Vitendo vya kuunga mkono |
|---|---|
| **Jifunze jina la kila mmoja** | Tengeneza chati ya kukaa, tumia majina yao kikamilifu na watake wanafunzi wakae katika viti/nafasi kwa angalau mwanzo wa kila somo kwa wiki chache za kwanza. |
| | Cheza michezo shirikishi ya ‘kukujua’ au taja michezo ili kila mmoja ajifunze jina la mwenzake, na wanafunzi wabadilishane masomo machache ya kwanza ili kujitambulisha kwa darasa zima mwanzo wa kila somo. |
| | Tumia kadi za majina na vitambulisho na washirikishe na wanafunzi wote kwa usawa. |
| **Washirikishe wanafunzi katika kuanzisha darasa lenye utaratibu** | Teua ‘wasaidizi wa darasa’ wakusaidia kwa kuonesha, kutoa nyenzo nk. |
| | Wafunze wanafunzi wote katika majukumu mahususi ya kuongoza kujifunza kwa kikundi kuandika kumbukumbu, kutunza muda, kuripoti. |
| | Mtake mwanafunzi, kwa usaidizi wako, atengeneze kanuni za darasani, kusaini na kuonesha. |

| | |
|---|---|
| **Mpitie mwanafunzi mmoja mmoja** | Fuatilia maendeleo na fanya upimaji awali mapema ili ujuwe ni wanafunzi gani wanahitaji msaada wa ziada. |
| | Unapoguswa kuhusu utendaji kazi au mabadiliko ya tabia, fanya mkutano wa kibinafsi na mwanafunzi katika nafasi tulivu na ya siri. |
| | Unda wasifu wa mwanafunzi unaojumuisha habari kuhusu maisha ya nyumbani ya mwanafunzi. |
| **Himiza mazungumzo** | Mpe kila mwanafunzi nafasi ya kuzungumza darasani katika wiki chache za kwanza ili kuwahamasisha kushiriki katika mijadala ya darasa zima. |
| | Himiza maswali na maoni ‘kuwa msikivu na mchangamfu na toa muongozo na muda wa kujibu kwa wanafunzi wakimya zaidi. |
| | Kubali kwamba jambo fulani ni gumu kabla ya kuwataka wanafunzi kujibu maswali magumu, na wafanye wahisi ni sawa kufanya makosa. |
| **Kuwa ni mwenye kupatikana** | Tenga dakika 10-15 wakati mwengine wa siku ili kuona wanafunzi wanaotaka kuuliza maswali au kujadili kazi kwa undani zaidi. |
| | Jihusishe na shughuli za ziada za masomo. |

**Majibu kwa mkufunzi:**

- Kadi za ‘kitendo saidizi’ katika safu wima ya kulia zimepangwa kando ya kadi za ‘majukumu ya kupanga’.

## Kielelezo nambari 6.10: Video ya EENET ‘Siku ya mjumuisho’, Mpango wa 7 juu ya ufundishaji na ujifunzaji.

Nenda moja kwa moja kwenye video kwenye YouTube yenye urefu wa dakika 13:

www.youtube.com/watch?v=KyheWrstoHU

Au tembelea tovuti ya EENET’s ili kujua zaidi kuhusu video na kupata kuona na kupakua:

www.eenet.org.uk/the-10-videos-and-manuals/

## Kielelezo nambari 6.11: Dondoo muhimu kutoka kwenye nakala ya video

- Katika kila somo, unaweza kutumia aina mbalimbali za vitendo. Panga kutumia vitendo zinavyohusisha kutazama, kusikiliza, kuzungumza, kugusa na kutembea. Aina hizi mbalimbali za vitendo vinamaanisha kuwa unaweza kurekebisha kila somo ili kuendana na matakwa na uwezo tafauti wa wanafunzi.

- Fanya masomo yawe ya kufurahisha. Anza kwa kuwa mwalimu mwenye furaha na mwenye tabasamu. "Ikiwa walimu wana nyuso zenye tabasamu na nia njema kwetu tunajisikia vizuri…wanacheza michezo na sisi na haya yanatia nguvu akili zetu na tunafahamu zaidi."

- Wanafunzi hujisikia vizuri zaidi kwa kuona wamejumuishwa ikiwa masomo wanayojifunza yanaonekana kuendana na maisha yao. Kuna njia nyingi za kuleta maisha halisi katika darasa. Unaweza ukatumia vitu vinavyopatikana nyumbani. Unaweza ukatumia vitu vinavopatikana katika mazingira. Mafunzo mradi yanasaidia kuunganisha masomo na maisha halisi. Unaweza pia kutumia igizodhima kulileta somo kwenye maisha.

- Unaweza kutumia nafasi nje ya darasa kufanya masomo yawe yameunganishwa zaidi na jamii au mazingira. "kama wanakwenda nje wanayo nafasi ya kupumzisha akili zao. Ikiwa wanakaa darasani na mwalimu anazungumza muda wote, watalala".

- Baadhi ya wanafunzi hujifunza vizuri zaidi wanapofanya kazi pamoja katika vikundi au katika jozi. "Kazi ya kikundi inamaanisha wanafunzi watashirikiana kubadilishana mawazo yao ili kuunda kitu kizuri. Kazi ya kikundi pia itawaruhusu wanafunzi kukubaliana. Kwasababu kuna wanafunzi wenye ulemavu katika kikundi, wanaweza kuelewana vyema zaidi. Kazi ya kikundi huwafurahisha wanafunzi, na mimi, nafurahi nikiwaona wanafunzi wanaendelea na kupata jambo fulani".

- Wanafunzi hujifunza mengi kutokana na kujifunza wao kwa wao.

- Unaweza kutumia mbinurika za kujifunza ili kuleta tafauti katika masomo. "Moja ya kielelezo kikubwa katika mazingira ya skuli ni wanafunzi

wengine…”. Ujifunzaji rika unaweza kuwa muhimu hasa katika madarasa yenye wanafunzi wengi.

- Tumia vitabu vya kiada kiubunifu. Unaweza kuwahimiza wanafunzi kusoma pamoja kwenye vitabu na kujadili yaliyomo. Unaweza kumuweka pamoja mwanafunzi anayesoma na kufahamu vizuri na mwanafunzi anayehitaji msaada zaidi.

- Toa msaada binafsi kwa wanafunzi wanaouhitaji. Tumia muda kuchunguza darasa ili kuona ni nani anahitaji usaidizi zaidi.

- Wapa wanafunzi maoni chanya na ya kutia moyo, hata kama wamekosa kitu fulani inaweza kuwasaidia kujisikia wameshirikishwa na wamehamasishwa kujifunza.

## Kielelezo nambari 6.12: Mbinu za kujifunza kwa vitendo

| Mawazo/mikakati iliyotumika | Maoni |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

## Kielelezo nambari 6.13: Malengo ya ujifunzaji

Nakili na ukate kadi hizi za lengo la kujifunza na uwape kila kikundi kadi tafauti.

| **Lugha** | **Hisabati** |
|---|---|
| Anza kutumia vihusishi vya wakati, mahali na maana yake, kwa mfano,<br>• Saa sita,<br>• Ninaishi Chakechake<br>• **Kwenye nambari** 23<br>• **Kwa** mstari<br>• **Kwa** mashua… | Kuonesha dhana ya:<br>(i) Nzima, (ii) Nusu, (iii) Robo, (iv) Theluthi<br><br>Ili kuzipanga dhana hizi kutoka ndogo hadi kubwa na kubwa hadi ndogo na kuelewa maneno ‘ndogo’ na ‘kubwa zaidi’. |

| | |
|---|---|
| **Sayansi/Mimea**<br><br>Kufahamu athari za maji, joto na mwanga kwenye ukuaji wa mimea. | **Masomo ya kijamii/Jografia**<br><br>Kuelezea jinsi hali ya hewa inavyoathiri hali ya maisha katika eneo la wanafunzi. |
| **Sayansi/Afya na ukuaji**<br>Kuelewa kuwa kufanya mazoezi na kula aina sahihi na kiasi cha chakula huwasaidia wanadamu kuwa na afya njema. | **Masomo ya jamii /Historia**<br>Lenga kufahamu mpangilio wa matukio, vipindi vya wakati vya historia na jinsi vipindi vya wakati vinavyo ainishwa. |

# Kielelezo nambari 6.14: Mikakati ya ujifunzaji mahiri

Ujifunzaji mahiri unahusisha ushirikishwaji wa wanafunzi kikamilifu katika mchakato wa kujifunza. Katika kujifunza kwa vitendo, kuna msisitizo mkubwa zaidi katika ujuzi wa kutatua matatizo, kukuza stadi za uchambuzi na kufikiria kwa kina. Kwa hivyo, mikakati hai ya kujifunza inahusisha wanafunzi kufanya mambo mara nyingi kwa pamoja, na kufikiria juu ya kile wanachofanya. Kwa hivyo, ujifunzaji mahiri unatoa fursa kubwa zaidi ya maoni.

Ifuatayo ni orodha ya aina za vitendo ambavyo walimu wanaweza kuvitumia, kwa urahisi, ili kuhimiza kujifunza kwa bidii. Haya yanahitaji kupangwa ili kukabiliana na mahitaji ya wanafunzi, maslahi, na kiwango kilichopo cha maarifa na uzoefu.

1. Kutumia vitu bandia au vitu vya Sanaa.
2. Kubungua bongo
3. Kutumia kazi za jozi na vikundi
4. Kutoa fursa kwa wanafunzi kutumia lugha yao ya kwanza ambapo inasaidia kuelewa (Kwa mfano, kutoa taarifa na lebo katika lugha yao ya kwanza)
5. Kutoa taswira zinazosaidia upatikanaji wa msamiati.
6. Mijadala ya vikundi na utatuzi wa matatizo shirikishi.
7. Kutumia majaribio
8. Dhana ramani
9. Wanafunzi wanaoongoza: Kuchagua, Ufundishaji rika, kutafiti na /au uwasilishaji.
10. Kutengeneza bango au kipande chengine cha kazi kwa ajili ya kuonesha
11. Kutumia michezo, chemshabongo au mafumbo.
12. Kutumia igizodhima, tamthilia na/au utendaji.
13. Kutumia nafasi za nje.

## Kielelezo nambari 6.15: Faida na changamoto za kazi ya kikundi

| Faida za kazi ya kikundi | Changamoto za kazi ya kikundi |
|---|---|
| • Huongeza ushiriki<br>• Kujifunza kutoka kwa kila mmoja<br>• Hukuza kuzungumza/kusikiliza<br>• Hukuza ujuzi wa mawasiliano ya kijamii<br>• Ushirikiano/kazi ya pamoja<br>• Hukuza ujifunzaji mahiri<br>• Hukuza umakini<br>• Huongeza uwezo wa kufikiri na kutatua matatizo<br>• Mwingiliano mkubwa wa mwalimu pamoja na wanafunzi<br>• Kujitegemea kwa mwanafunzi<br>• Kuhamasisha na kujishughulisha<br>• Hukuza ujuzi wa uongozi<br>• Inabadilisha kasi ya kujifunza<br>• Hukuza uwelewa<br>• Fursa kubwa zaidi za upimaji | • Inaweza kuwa vigumu kuhamisha samani za darasani ili kushughulikia kazi ya kikundi yenye ufanisi<br>• Inaweza kuwa na kelele<br>• Wanafunzi wanaweza wasiende<br>• Wanafunzi wanaweza kuacha<br>• Kazi ngumu kwa mwalimu kufuatilia kila mwanafunzi<br>• Inachukuwa muda mwingi<br>• Wanafunzi wengine wanaweza kuacha kazi kwa wengine<br>• Wanafunzi kikawaida wanaweza kupangwa na wanafunzi wale wale<br>• Vikundi vyengine vinamaliza vizuri kabla ya vingine |

# Kielelezo nambari 6.16: kupanga muundo wa kila kikundi

Nakili na ukate kadi hizi na uwape seti kwa kila kikundi

| Kazi | Vikundi vyenye uwezo tafauti, lengwa au wenye uwezo sawa? | Kwa nini? |
|---|---|---|
| Kufanya jaribio la sayansi ambalo linahusisha uchunguzi wa nje na kuwasilisha. | **Uwezo tafauti** | *Ili wanafunzi wote wajifunze kutoka kwa kila mmoja wao na kuleta ujuzi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya kazi.* |
| Kujitayarisha kwa mjadala wa darasani kama pesa ungekua bora bila elimu. | **Uwezo tafauti** | *Ili watu wenye mazingira, mawazo na uzoefu tafauti waweze kutoa hoja zao.* |
| Kuwasaidia wanafunzi waliochelewa kuanza muhula wa skuli ili wafikie. | **lengwa** | *Hivyo wana nafasi ya msaada wa ziada kwa vile wako nyuma.* |
| Kudurusu kwa ajili ya mitihani ya nje kwa kujadili maswali mbalimbali kuhusu mada fulani. | **Uwezo sawa** | *Kwa hivyo wanaweza kuzingatia maswali na kufanya kazi katika kiwango ambacho wanahitaji kufanya.* |
| Jukumu lako | | |

**Majibu kwa mkufunzi:** Kadi za 'Uwezo' na 'kwa nini?' zimepangwa katika safuwima za mkono wa kulia kando ya kadi za 'kazi' zinazosaidia.

## Kielelezo nambari 6.17: Orodhahakiki ya kupanga kazi ya kikundi bora

| | |
|---|---|
| Je! Kazi ni maalumu na wazi? | |
| Je! kazi hii inafaa kwa kazi ya kikundi (inayohusisha utatuzi wa matatizo, kufahamu dhana mpya, uchunguzi/utafiti au ufahamu)? | |
| Je! Umepanga jinsi ya kuunda vikundi? Je! Unajali maswala ya jinsia na ujumuishi, kuhakikisha kila mmoja anashiriki? | |
| Je! Umetoa hesabu kuhusu vizuizi kwa harakati za wanafunzi katika darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi? | |
| Je! wanafunzi wote watashiriki? | |
| Je! umepanga wanafunzi katika kila kikundi kushikilia majukumu mahususi? | |
| Ikiwezekana, umepanga kwa ajili ya mwanafunzi mkubwa au mtu mzima mwengine aje kusaidia? | |
| Je! Shughuli zimepangwa na vifaa vimetayarishwa? | |
| Je! darasa limefunzwa jinsi ya kuendesha kazi za kikundi au unahitaji kutenga muda wa kufanya hivi? | |
| Je! Umepanga jinsi vikundi vitakavyojibu kazi, kwa mfano, kupitia uwasilishaji, kuripoti nk? | |
| Je! Utakuwa wazi na mkali kwa kuweka muda ili kuhakikisha kasi na ushiriki? | |
| Je! Unapanga kuzunguka, kusaidia kujifunza, na kuona jinsi wanafunzi wanavyoshirikiana? | |
| Je! Una mpango wa kutumia fursa hii kwa uchunguzi na upimaji wa baadhi ya wanafunzi binafsi? | |

## Kielelezo nambari 6.18: Wajibu na Majukumu

Nakili na ukate kadi hizi na utoe seti kwa kila kikundi.

| Mwenyekiti | Mpokeaji madokezo | Mtangazaji | Mratibu na mtunza wakati |
|---|---|---|---|
| Kuhakikisha kuwa kazi inafahamika na kila mtu ana nafasi ya kuzungumza. | Huandika mambo muhimu kuhakikisha kwamba mwandishi wa habari anaweza kuyasoma | Kuliambia darasa zima kile ambacho kikundi kimesema au kufanya. | Anahakikisha kuwa kikundi kina vifaa vyote vinavyohitaji na kwamba vinazingatia wakati. |
| *'Nini unadhani'? unafikiria nini?' je! Yuko sahihi kusema nyenzo hii ni ya sumaku?'* | *'Wacha niangalie. Unatamkaje shaba?'* | *'Tulidhani kwamba nyenzo nne zilikua za sumaku.'* | *'Hizi hapa kalamu.'* |
| *'Unafikiri kuna nini ndani ya vitu?'* | *'Je! Unaweza kuangalia kama hii ndio orodha yetu ya mambo tuliyokubaliana?'* | *'Tuliamua mvutano si jaribio zuri ikiwa nyezo ni sumaku '* | *'Nitaleta vitu vya ziada'* |
| *'Umesema sana. Acha mwengine aseme.* | *'Je! Napaswa kuweka ile mwanzo au mwisho?'* | *'Tuliona ni vigumu sana kuamua kwa sababu ....'* | *'Tuna dakika moja tu.'* |
| Ongeza mifano yako mwenyewe | Ongeza mifano yako mwenyewe | Ongeza mifano yako mwenyewe | Ongeza mifano yako mwenyewe |

## Kielelezo nambari cha 6.19: Kanuni za darasani kwa kazi ya kikundi

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mashirikiano | Fanya kazi kwa bidii muda wote | Daima fanya kazi kama kikundi | Saidianeni |
| Zungumzeni na sikilizaneni kwa makini | Sikiliza maagizo | Badilishaneni mawazo | Jadili mambo kimya kimya |
| Jaribu kumfikia kila mtu katika kikundi | Uwe na busara | Kuwa na furaha kufanya kazi na kila mmoja katika kikundi | Jaribu kukubaliana na kila mmoja |
| Kuwa na vifaa sahihi | Heshimu maoni ya kila mtu. | Zunguka darasani kwa uwangalifu bila ya kukatiza masomo ya wengine | Kuwa tayari kuchukua jukumu lolote na uwatie moyo wengine wafanye hivyo pia. |
| Ongeza mifano yako mwenyewe | Ongeza mifano yako mwenyewe | Ongeza mifano yako mwenyewe | Ongeza mifano yako mwenyewe |

## Kielelezo nambari 6.20: Orodhahakiki ya kuendesha kazi ya kikundi yenye mafanikio

| | |
|---|---|
| Je, wanafunzi wanajua pakwenda wanapohamia katika vikundi? | |
| Je, wanafunzi wanajua la kufanya? Je! kazi ni maalumu na maelekezo yako wazi? | |
| Je, umeanza kwa uwazi malengo ya kazi ya kikundi? | |
| Je, Unatekeleza ipasavyo matarajio ya kikundi? | |
| Je, unaruhusu maswali ili kila mtu awe wazi kuhusu jukumu hilo? | |
| Je, darasa linajua ni mkono gani unaashiria/kuamuru kuangalia/kusikiliza kwa hivyo wanajua wakati wa kuacha kuzungumza? | |
| Je, kila mtu yuko wazi kuhusu muda na kuambiwa mara kwa mara ni muda gani uliobakia? | |
| Je, umetayarisha kazi ya ziada kwa wanafunzi wanaomaliza mapema? | |
| Je, kuna fursa kwa vikundi kutoa maoni au kuwasilisha kazi zao? | |
| Je, unazunguuka darasani ili kuona maendeleo na matatizo gani yanakuja?<br>Je, unatoa ushauri, unashajiisha, na kutoa msaada binafsi pale unapohitajiaka? | |

## Kielelezo nambari 6.21: Mikakati ya kuweka katika vikundi kwa madhumuni mbalimbali

| Jina la mkakati | Ni nini? | Kwa nini utumie? |
|---|---|---|
| **Fikiri, Jozisha, shirikisha** | Wanafunzi hufikiria mmoja mmoja kuhusu swali/ tatizo, ungana na mtu kujadili mawazo yao kisha wabadilishane mawazo yao na kikundi chao cha meza nahatimaye kikundi kizima. | Wanafunzi hutumia maarifa yao ya awali na kubadilishana mawazo yao na wenzao. Hii inawapa wanafunzi nafasi ya kupanga mawazo yao kabla ya kuyawasilisha kwenye kundi kubwa zaidi. |
| **Geuka na uzungumze** | Mwalimu anauliza darasa na wanafunzi wanamgeukia mtu aliekaribu nae ili kujadili. | Wanafunzi wanaweza kubadilishana mawazo yao na wengine na kutumia ujuzi wao wa awali kuhusu mada. |
| **Changanya kete** | Kama ilivyo mbinu ya changanyakete iliyokamilika, kila mwanafunzi katika kikundi cha 'changanyakete' ana jukumu la kujifunza kipande cha habari/mada. Wanafanya hivi katika 'kikundi cha wataalamu' wa muda kabla ya kurudi kwenye kikundi chao cha 'nyumbani' ambapo washiriki kwa timu hufundishana walichojifunza. Hii inawawezesha wote kufahamu habari yote. | Inahimiza ushirikiano huku ikikuza stadi za kusoma/kufahamu. Inasaidia kujenga tabia njema kwa kuwashirikisha wanafunzi na inahitaji kazi ya pamoja yenye ufanisi kutegemeana na ujuzi mwengine baina ya watu. |

| | | |
|---|---|---|
| **Bakuli la samaki** | Wanafunzi wachache hukaa katikati ya kikundi cha majadiliano ya 'bakuli la samaki' na wanafunzi waliobakia hukaa karibu nao. Wanakikundi cha majadiliano hujibu maswali yaliyotolewa na kubadilishana mawazo yao. Wanaweza pia kujibu maswali yanayoulizwa na kundi kubwa. Wanafunzi huzunguka ndani na nje ya kikundi cha majadiliano ya bakuli la samaki. | Inafaa kwa vikundi vikubwa na inaweza kuhusisha kila mmoja. Inawaonesha wanafunzi jinsi mjadala mzuri unavyokua. Inaweza kufanya shughuli bora ya uandishi wa awali kuruhusu wanafunzi kuchunguza maswali au mawazo kwa undani zaidi kabla ya kila mwanafunzi kufanya kazi ya pekee. |
| **Pembe nne** | Wanafunzi wanaonesha msimamo juu ya kauli maalumu ('Kukubali sana', 'kukubali', kukataa', 'kutokubali kabisa'). Kwa kusimama katika kona ya chumba iliyoainishwa kwa kila kauli. | Shughuli hii inahitaji kila mmoja kuchukua nafasi. Ni amsha amsha nzuri ya shughuli ambapo wanafunzi hujibu taarifa kuhusu mada watakayojifunza. Pia, inaweza kuwa shughuli ya ufuatiliaji wakati wanafunzi wanapotumia yale waliojifunza. |
| **Mzunguko wa Robin** | Wanafunzi huunda vikundi vya watu watatu au wanne. Wanapitisha karatasi na kila mwanafunzi anaandika habari kwenye karatasi mpaka muda utakapomalizika au wawe wamefikia idadi fulani ya maigizo kuhusu mada. | Hii inahusu wanafunzi kubadilishana maarifa yao kwa njia isio ya vitisho na pia kuona kile ambacho wanafunzi wenzao wanajua. |

| | | |
|---|---|---|
| **Matembezi ukumbini** | Maswali/matatizo yanaandikwa kwa kalamu katikati ya karatasi kubwa (Ya ukubwa wa A3/A2). Hizi zimewekwa kwenye meza tafauti au mahali tafauti kwenye kuta. Wanafunzi huunda vikundi vingi kadiri ya maswali, na kila kikundi huhama kutoka swali hadi swali. Baada ya kuandika jibu lao kwa swali la kwanza mahali popote kwenye karatasi, kikundi huzunguka hadi nafasi inayofuata, na kuongeza kile ambacho tayari kipo. Katika swali la mwisho, ni jukumu la kikundi kufanya muhutasari kwa kile kilichoandikwa na kikundi na kutoa ripoti kwa darasa. | Hii inakuza ushirikiano, ujuzi wa kusikiliza, na kujenga timu. Inawahusisha wanafunzi kikamilifu na inawasaidia kujifunza jinsi ya kufikia makubaliano, njia za kuandika majibu yao na jinsi ya kufupisha na kuripoti kwa darasa zima. |
| **Maduara ya mazingatio** | Wanafunzi husimama katika maduara mawili wakitazamana na kujibu swali katika majadiliano ya jozi. Inaposhitukizwa na mwalimu, duara moja husogea kwenda kushoto au kulia ili kila mwanafunzi sasa akabiliane na mwenza mpya, ambae wanajadiliana swala jipya | Mbinu hii humwezesha kila mwanafunzi darasani kushiriki kama msikilizaji na mzungumzaji hai. Huwachanganya wanafunzi ili wapate fursa ya kushiriki na wanafunzi mbalimbali. Kwasababu wanazungumza na mtu mwengine mmoja tu kwa wakati, wanafunzi wenye haya wanaojitenga wanaweza kujisikia vizuri zaidi kuchangia mawazo yao kuliko wangefanya katika majadiliano ya kikundi au darasa zima. |

# Kielelezo nambari 6.22: Utafautishaji wa usaidizi hatua kwa hatua

Nakili na ukate kadi hizi na utoe seti kwa kila kikundi.

| Usaidizi hatua kwa hatua | Utafautishaji |
|---|---|
| Maandishi yamegawanywa 'vipande vipande' ili darasa lisome kipande kimoja kwa wakati mmoja. | Toleo lililorahisishwa na matini inayosomwa kwa baadhi ya wanafunzi. |
| Somo la jinsi ya kuendeleza mabishano kabla ya kutakiwa kuandika insha ya mazungumzo. | Kuwekwa kwa jozi na mwanafunzi ambae anajua jinsi ya kutumia nukuu. |
| Onesha jinsi ya kufanya mlingano wa hisabati ubaoni | Toa ufafanuzi wa jinsi ya kufanya mlingano wa hisabu kwa maandishi yaliokuzwa kama kitini. |
| Ili kujiandaa kwa swali la insha ya historia, darasa huchunguza chanzo cha kihistoria ili kubainisha mambo matatu wanayoyoweza kuyaona na mambo matatu wanayoyoweza kudhania | Kijitabu chenye orodha ya mambo kumi kimetolewa kwa baadhi ya wanafunzi... na wanatakiwa kuchagua vitu kutoka kwenye orodha ambavyo vinaweza kuonekana au kukisiwa kutoka kwenye chanzo fulani cha kihistoria. |
| Somo la msamiati kabla ya darasa kusoma matini ngumu. | Maneno muhimu kutoka kwenye matini ngumu hutafsiriwa katika lugha ya kwanza ya wanafunzi. |
| Mwanzoni mwa mada, mwalimu anawambia wanafunzi wabadilishane uzoefu au mawazo yao wenyewe kuhusu maudhui au dhana ya somo ili walete kile ambacho tayari wanachokijua kwenye somo. | Mwanafunzi yeyote ambaye alikosa masomo ya awali yanayohusiana na mada mpya hupewa muhtasari maalumu kuhusu masomo hayo kabla ya somo jipya |

**Majibu kwa mkufunzi:** Kadi zimepangwa chini ya kichwa cha habari (Kwa herufi zilizokozeshwa kinachoeleza ni mkakati wa aina gani, na kando ya mkakati wa lengo lile lile la kujifunza.

## Kielelezo nambari 6.23: Utafautishaji wa kujumuisha uwezo tafauti

| | |
|---|---|
| **Mikakati ya kutafautisha kwa viwango vya uwezo wa juu** | • Toa muda wa ziada au shughuli zenye changamoto zaidi.<br>• Himiza ushirikiano na kujifunza rika katika vikundi vya uwezo mchanganyiko.<br>• Tumia wanafunzi wenye uwezo wa juu kama walimu rika au washauri.<br>• Toa maelekezo kwa vikundi wakati wa somo. |
| **Mikakati ya kutafautisha kwa viwango vya uwezo wa kati** | • Weka mafunzo katika viwango vya uwezo wa kati.<br>• Himiza ushirikiano na ujifunzaji rika katika vikundi vya watu wenye uwezo tafauti.<br>• Wape wanafunzi shughuli ya ziada ikiwa watamaliza mapema. |
| **Mikakati ya kutafautisha kwa viwango vya chini vya uwezo** | • Fikiria ujifunzaji wa msingi unaohitajika na urekebishe au kurahisisha nyenzo za kuegemea ili mafunzo yaweze kufikiwa.<br>• Toa vipindi vya maandalizi ya kabla ya kufundisha na baada ya kufundisha na vipindi vya mapitio ya ufundishaji kabla/ baada ya darasa.<br>• Toa mifano kadhaa.<br>• Toa maagizo ya hatua kwa hatua.<br>• Usaidizi wa msamiati katika lugha ya kwanza ya mwanafunzi.<br>• Himiza ushirikiano na ujifunzaji rika katika vikundi vya uwezo mchanganyiko.<br>• Tumia walimurika au washauri.<br>• Toa maelekezo kwa vikundi wakati wa somo. |

## Kielelezo nambari 6.24: Mpango wa utafautishaji

| | |
|---|---|
| Mada ya somo/lengo la kujifunza | |
| Mkakati hai wa kujifunza kutoka kipindi cha 6.3 | |
| Je! Utarekebisha vipi vitendo kwa wanafunzi ambao wana uwezo mdogo? | |
| Je! Utarekebisha vipi kitendo ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye uwezo mkubwa wanashiriki kikamilifu? | |

## Kielelezo nambari 6.25:  Video ya EENET'Siku ya mjumuisho', Programu ya 4 juu ya uandaaji wa masomo

Nenda moja kwa moja kwenye video kwenye YouTube. Ina urefu wa dakika 6:

www.youtube.com/watch?v=E27Nn_JT1ls

Au tembelea tovuti ya EENET's ili kujua zaidi kuhusu video na upakuwe viungo vya kufikia na kutizama:

www.eenet.org.uk/the-10-videos-and-manuals/

# Kielelezo nambari 6.26: Nakala ya video

**Kuandaa masomo**
Kila mwanafunzi hujifunza kwa njia na kasi tafauti. Walimu wa mjumuisho hujibu kwa urahisi mahitaji mbalimbali ya wanafunzi katika madarasa yao. Unaweza kujibu vyema mahitaji ya kila mwanafunzi ikiwa umejitayarisha vyema kabla ya kila somo.

**Unaweza kufanya nini?**

Je, lengo linahusiana a na mtaala?

“Mwalimu anapaswa kujiandaa vyema na kila wakati afikirie mbele juu ya kile anachokwenda kukifundisha.”

Tambua ni vitendo gani utafanya ili kuwasaidia wanafunzi kujifunza kile unachotaka wajifunze.

“Wakikaa tu na kuandika, wanasinzia lakini tunapofanya vitendo wanafurahi kujifunza,  hawana usingizi na hawachoki”.

Utahitaji kuamua jinsi ya kurekebisha vitendo hivi kwa wanafunzi maalumu katika darasa lako. Kwa mfano, unaweza kuhitaji kurekebisha vitendo kwa wanafunzi ambao hawawezi kuona, kusikia, au kutembea vizuri sana. Huenda ukahitaji kuandaa baadhi ya vitendo rahisi zaidi au gawanya kazi katika hatua ndogo zaidi, kwa wanafunzi ambao wana shida ya kuelewa na kukumbuka.

Kabla ya somo kuanza, unahitaji kupanga vitabu vyovyote, nyenzo za kuandikia, na vitu vingine utakavyotumia. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinaweza kuwa vitu ulivyokusanya au kutengeneza bila malipo, kwa kutumia vitu ambavyo kwa kawaida hutupwa, kama vile masanduku ya kadi bodi, au vifuniko vya chupa.

“Ni muhimu kuandaa masomo mapema na kuhakikisha vifaa vinavyohitajika vitapatikana kwa ajili ya somo unalokwenda kufundisha, maandalizi hufanyika mapema sana, mara nyingi maandalizi hufanyika nyumbani ili uweze kukusanya vifaa unavyohitaji, si mara zote kwamba tunakuwa tunavyo vifaa tunavyohitaji skuli. Kwa vile tuna wanafunzi wenye ulemavu darasani, tunatakiwa

kuhakikisha tunatayarisha nyenzo ambazo wanaweza kutumia na kuchezea kwa ajili ya masomo. Kama sehemu ya maandalizi yako, unahitaji kuandika katika kitabu chako kila kitu ambacho utafanya na kutumia siku inayofuata.”

Unaweza kutengeneza visaidizi vya kufundishia na kujifunzia wewe mwenyewe. Unaweza pia kuwashirikisha wanafunzi katika kuvitengeneza. Kwa mfano, wanafunzi wakubwa wanaweza kusaidia kutengeneza nyenzo kwa ajili ya wanafunzi wa madarasa ya chini. Au wanafunzi wenye uwezo wa kuona wanaweza kutengeneza nyenzo za kugusa kwa ajili ya marafiki zao wenye uoni hafifu.

Unaweza kuimarisha upangaji wako wa somo, na kutengeneza nyenzo bunifu zaidi za kufundishia na kujifunzia, ikiwa unafanya kazi na walimu wengine. Unaweza kubadilishana mawazo na uzoefu, kuazimana nyenzo au hata kuweka jadweli la nyenzo au chumba cha nyenzo katika skuli yako.

"Katika skuli yetu kuna shughuli mbalimbali ambazo tunapanga kwa mwaka mzima unaokuja, tunapanga masomo kwa pamoja ili tusaidiane na kushirikishana katika masomo yetu.  Tunatoa maoni kuhusu jinsi tunavyoweza kuimarisha.

Inaweza kuwa changamoto kwa walimu kupata muda au nafasi ya kuandaa masomo. Walimu wakuu wanatakiwa kuhakikisha walimu wanapata muda katika ratiba ya kila siku ya kupanga. Ikiwezekana, wanahitaji pia kutoa nafasi skuli ambapo walimu wanaweza kufanya maandalizi yao.

# Kielelezo nambari 6.27: Msaada kwa wanafunzi wenye ulemavu

Nakili na ukate kadi hizi na ukipe kila kikundi kidogo cha wataalamu.

**KUONA**

Usaidizi rika/rafiki, taswira, mwangaza mzuri/mng'ao uliopunguzwa, vionesho vya ukutani, mabango, kadi, vipanga picha, uchapishaji/maandishi yaliyokuzwa, chati za mtiririko, ramani za mawazo, mbao kubwa za hadithi, vielelezo, panga kwa rangi, nukta nundu, shughuli za kugusa/usikivu, uwekaji wa viti.

**KUSIKIA**

Usaidizi rika/rafiki, usimulizi wa hadithi, kuigiza, kuifanya ionekane, marudio/kurudia, muziki, utungo, kazi ya kikundi, mahojiano, mawasilisho, kanda za sauti na vipokea sauti vinavyobanwa kichwani, video, kutia saini, kupunguza kelele ya chini chini, uwekaji wa viti.

**KUTEMBEA**

Rafiki wa kuchukua kumbukumbu, kazi ya kikundi, miondoko ya mikono, ubao na michezo ya kadi, fuata shughuli zilizokaa pamoja na kuzungukazunguka/ toa mapumziko, dhana za uandishi zilizorekebishwa, mazoezi ya kujaza mapengo/zoezi la kuoanisha, kuweka viti, usaidizi wa ziada wa kazi zinazohitaji ujuzi mzuri wa kutumia viganja vya mikono.

## Kielelezo nambari 6.28: Kurekebisha vitendo vya wanafunzi wenye ulemavu

| | |
|---|---|
| **Mada ya somo/lengo la kujifunza** | |
| **Vitendo** | |
| **Je! Utarekebisha vipi vitendo kwa wanafunzi wenye uoni hafifu?** | |
| **Je! Utarekebisha vipi vitendo kwa wanafunzi wenye usikivu mdogo?** | |
| **Je! Utarekebisha vipi vitendo kwa wanafunzi ambao hawawezi kutembea kwa urahisi?** | |

# Kielelezo nambari 6.29: Hatua za kusaidia ujifunzaji

| Majina ya wanafunzi na jinsi wanavyoendelea na kazi | Uingiliaji kati wa mwalimu uliopendekezwa |
|---|---|
| **Halima**<br>Halima hajaanza. Anasema hajui jinsi ya kuanza. | |
| **Hamad**<br>Hamad ameandika ukurasa mzima kwa dakika chache na ni wazi ana hadithi ya kusimulia. Lakini ni vigumu kufahamu kwani hakuna alama za uakifishi. | |
| **Mwana**<br>Mwana anashughulishwa na kucheza na bangili kwenye mkono wake. Alipoulizwa, alisema hawezi kufikiria muhusika mkuu wa hadithi yake. | |
| **Abdullah**<br>Abdullah amemaliza kile kinachoonekana kama hadithi nzuri iliyoandikwa vizuri unapomfikia. Amekaa akionekana ni mchofu. | |
| **Fatma**<br>Fatma anashughulika kuandika na haoneshi shida yoyote. | |

# Kielelezo nambari 6.30: Maoni muhimu

Toa mrejesho kwamba, yanapotumiwa ipasavyo, huimarisha ujifunzaji:

- Uwazi, kuwa mahsusi na bila ya kutumia istilahi za kitaalamu
- Maoni ya mdomo yanapaswa kuwa ya ukubwa wa saizi ya kiasi, si zaidi ya nukta tatu au nne muhimu.
- Mwaminifu
- Kutia moyo
- Sambamba
- Lengo
- Tathmini
- Kujenga
- Chanya
- Kubainisha uwezo pamoja na udhaifu wowote.
- Hutoa muongozo wa kweli na unaofaa kuhusu jinsi mwanafunzi anavyoweza kuboresha, kwa mfano:
- Mrejesho wa kina huanza kwa kusema kile mwanafunzi alichofanya vizuri, husonga mbele hadi maeneo ambayo mwanafunzi angeweza kufanya vizuri zaidi na kuishia kwa maoni chanya.
- Umeunganishwa hasa na kile kilichohitajika na kila kazi au kigezo cha upimaji.
- Haraka na kwa wakati.
- Unahakikisha siri inapofaa.

## Kielelezo nambari 6.31: Fanya na usifanye

“Hilo ni wazo zuri, na linaweza kufanyakazi vizuri zaidi ikiwa uta….”

“Sijui. Inaonekana ni ujinga kwangu….”

“Wanadarasa wengine wanafahamu kwa nini wewe hufahamu?”

“Nimeweka alama mahali ambapo umekosa kituo kikubwa au kidogo?”

“Sijali kama huna mstari wakati mwengine nataka vipimo sahihi?”

“Endelea, toa maarifa yako ya awali na uniambie umekusudia nini’”

“…Hatimaye, ulitakiwa kufanya muhutasari wa matokeo yako lakini hukufanya. Asha, unaweza kumuonesha yako kama mfano wa unavyoweza kufanya hivi. ……”

“…Ndio, kazi bado ni nyingi lakini nimefurahishwa sana na juhudi zako”

“Wasomee hii darasani ili waone jinsi ulivyo mvivu”

“Wiki iliyopita ulihangaika na hili lakini sasa unaweza….”

# Kielelezo nambari 6.32: Kadi za maoni za igizodhima

Nakili na ukate kadi hizi na wape kila kikundi kidogo seti za nyuso zilizoelekea chini.

| |
|---|
| **Mwanafunzi wa 1**<br>Wewe ni mwanafunzi utatakiwa kukamilisha kazi na mkufunzi. Anza kufanya kazi unapoambiwa tu. Wakati wa kazi, walimu wawili katika kikundi chako watakupa maoni yao. |
| **Mwanafunzi wa 2**<br>Wewe ni mwanafunzi utatakiwa kukamilisha kazi na mkufunzi. Anza kufanya kazi unapoambiwa. Wakati wa kazi, 'walimu' wawili katika kikundi chako watakupa maoni yao. |
| **Mwalimu wa 1**<br>Wewe ni mwalimu. Utawatazama wanafunzi wawili wanaofanya seti ya kazi na mkufunzi. Wakati wa kazi, kazi yako ni kutoa maoni yenye kujenga. Kuwa na taarifa. Wambie wanafunzi kile unachokiona na kugundua. Zungumza kuhusu kazi ambayo wamefanya, juhudi inayohusika, na (kuwawazia kama wanafunzi ambao umewafundisha kwa miaka mingi) maendeleo yoyote ambayo wamefanya (Kwa mfano, "Nakuona sasa unaweza..." "Wiki iliyopita ungeweza... lakini sasa unaweza..."). Mshawishi mwanafunzi "Azungumzie jinsi anavyohisi kuhusu kazi yake, kile anachofurahia zaidi na kile ambacho ni changamoto zaidi, na kama ni bora kuliko hapo awali.<br>**Kumbuka!** Fikiria kuhusu shughuli ambayo tumemaliza hivi punde kuhusu kile cha kusema tunapotoa maoni. Zingatia maswali mawili unapotoa maoni yako: unataka mwanafunzi afanye nini**?** Je! unataka mwanafunzi ajifunze nini? |
| **Mwalimu wa 2**<br>Wewe ni mwalimu. Utawatazama 'wanafunzi' wawili wanapofanya 'kazi' iliyowekwa na mkufunzi. Wakati wa kazi, kazi yako ni kutoa maoni hasi. Zingatia kile ambacho kila mwanafunzi anafanya vibaya. Zungumza kuhusu kile unachopenda kibinafsi, linganisha kazi ya 'wanafunzi' na ujivunie jinsi wanafunzi wengine ambao wamekua bora zaidi kuliko wengine. Fanya maamuzi kuhusu juhudi zao.<br>**Kumbuka!** Tumia mifano katika shughuli ambayo tumemaliza hivi punde kuhusu nini cha kusema wakati wa kutoa mrejesho. |

## Kielelezo nambari 6.33: Maswali bora

**Maswali bora …**

1. …Maslahi, kujihusisha na changamoto
2. …imarisha ujifunzaji uliopita.
3. …kufichua ufahamu au dhana potofu.
4. …wanafunzi kupitia mfuatano uliopangwa ambao hatua kwa hatua huweka ufahamu muhimu.
5. …zingatia kufikiri juu ya dhana na maswala muhimu.
6. …panua fikra kutoka kwenye ukweli/uhalisia hadi uchambuzi/upimaji.
7. …himiza majadiliano na mjadala
8. …hitaji maelezo
9. …himiza ubunifu wa kufikiri na utatuzi wa matatizo.
10. …Wape wanafunzi ujasiri wa kutoa maoni yao.

# Kielelezo nambari 6.34: Baadhi ya mikakati ya kuuliza maswali

## 1. Toa majibu mbalimbali

Hii inajumuisha kuuliza maswali na kutoa majibu mbalimbali yanayowezekana-ambayo ni pamoja na majibu ya ndio, majibu ya uhakika hayana utata.

> Kwa mfano: bunge linafanya nini? a) Kutunga sheria. b) Kusimamia sheria. c) Kuimarisha maisha yetu. d) kuwafanya masikini kuwa masikini zaidi.

**Ili kuhakiki ujifunzaji**, mwalimu anawataka wanafunzi kuashiria wanafikiria jawabu ni ipi. Kutokana na hili mwalimu anajua kama wamejifunza au wanahitaji mafundisho zaidi.

**Kuimarisha ujifunzaji na kukuza fikra,** mwalimu huwaweka wanafunzi wenye majibu sawa kwenye kikundi, wanakwenda kwenye kona ya chumba na kupanga pamoja jinsi watakavyoweza kushawishi wanafunzi kwa upande mwengine kwamba wamekosea.

## 2. Geuza swali liwe kauli ya kweli au ya uongo.

Hii inahusisha kubadilisha swali kuwa kauli ya uchochezi na kuwataka wanafunzi washirikiane katika jozi kutumia mitazamo tafauti na kutumia kile wanachokijua kuhoji katika jambo hilo.

> Kwa mfano: Je! unakubali au hukubaliani na…?

Maswali yamefungwa yenye jibu sahihi hayana ufanisi kwa vile yanahitaji maelezo.

## 3. Usiulize swali-toa jibu na uulize kwanini ni sahihi au zingatia jinsi ya kutoa jibu

Hii inahusisha kuwapa wanafunzi jibu na kuwauliza jinsi wanavyofikiri jibu linaweza kuwa limefikiwa, au kwa nini wanafikiri ni sahihi. Hii inabadilisha muelekeo kutoka kwenye jawabu na kujadili **sababu** za jawabu.

> Kwamfano: a) Badala ya kuuliza 20÷3 ni ngapi, wambie waeleze **kwa nini** 20÷3 ni 6.66. Au b) badala ya kuuliza kama Ngamia wanafaa zaidi

kuishi sehemu zenye joto au baridi, uliza **kwa nini** Ngamia wanafaa zaidi kuishi sehemu zenye joto.

## 4. Uliza maswali yanayohamasisha uchunguzi

Wahimize wanafunzi kulinganisha na kutafautisha, kufikiri juu ya kile kinachofanana na kile ambacho ni tafauti, kuainisha na kuangalia mapungufu. Zinaweza kutumika kama kichocheo cha darasa, kikundi au majadiliano ya jozi.

Kwa mfano: Kwa nyasi ya Pampas ni gugu na Boogainvillea sio? Au: Kati ya yote ambayo tumejifunza kwenye muhula huu, ni nini kitakachokufaa zaidi ukiwa mtu mzima? Kwa nini?

# Rejea

UNESCO (2015) Vidokezo na Vitendo vya kufundisha madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi*: muongozo wa mwalimu* Bangkok: UNESCO (Ilipitiwa April 2022, https://www.eenet.org.uk/resources/docs/ilfe/generic/Sp2.pdf); Kutoka 'Embracing Diversity: Toolkit for Creating Incl usive, Learning-Friendly Environments Toolkit (inayopatikanwa kwenye tovoti ya EENET's: https://www.eenet.org.uk/ilfe-toolkit/).

Andria Zafirakou (2018). Global Teacher Prize winner
(Angalia www.youtube.com/watch?v=BrMaive-xiU)